# VIGEZO VYA UTOAJI WA MAJINA YA WATU KATIKA JAMII YA WAMATENGO

**ELVIS REGNARD MBUNDA**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI ISIMU) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2023**

# ITHIBATI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayoitwa **"*Vigezo vya Utoaji wa Majina ya Watu katika Jamii ya Wamatengo*"** kwa ajili ya kukamilisha sehemu ya masharti ya shahada ya (M.A Kiswahili - Isimu) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Dkt.Hadija Jilala

**(Msimamizi)**

Tarehe

## HAKIMILIKI

Haki ya kunakili tasnifu hii inalindwa na Mkataba wa Berne, sheria ya haki ya kunakili ya mwaka 1999 na mikataba mingine ya sheria za kitaifa na kimataifa zinazolinda mali za kitaaluma. Hairuhusiwi kukaririwa kwa mbinu yoyote ya kielektroniki kama kunakili, kutoa kopi au kurudufu sehemu yoyote ya tasnifu hii bila ya idhini kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba yake.

# TAMKO

Mimi **Elvis Regnard Mbunda,** ninatamka na kuthibitisha kwamba tasnifu hii ya utafiti iitwayo **"*Vigezo vya Utoaji wa Majina ya Watu katika Jamii ya Wamatengo*"** ni kazi yangumwenyewe na haijawahi kutolewa popote pale kwa lengo la kutunukiwa shahadayoyote katika Chuo Kikuu chochote.

______________________

Saini

# TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu **Bw. Regnard Yohannes Mbunda** na **Bi Daria Damas Nchimbi** kwa malezi yao mema waliyonilea na kunipa nafasi ya kusoma na kuwezesha kiuchumi hadi kufikia mafanikio haya ya kitaaluma.

## SHUKRANI

Matokeo na mafanikio ya kazi hii yametokana na michango na mawazo ya watu na taasisi mbalimbali. Kwa hakika si rahisi kumtaja kwa jina kila aliyehusika. Hivyo, nalazimika kuwataja wachache kwa niaba ya wote walioshiriki kwa namna moja ama nyingine kufanikisha utafiti huu.

Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, afya na akili njema iliyonisaidia kuifanya kazi hii kwa wepesi. Kwa hakika, bila uwezo wake, nisingeweza kuendelea na masomo, kufanya utafiti na mwisho kuandika tasnifu hii.

Pili, namshukuru sana msimamizi wangu Dkt.Hadija Jilala kwa juhudi zake kubwa za kuniongoza katika kufanikisha kazi hii. Alinivumilia katika madhaifu mbalimbali yaliyokuwa yakijitokeza kwangu kama binadamu na mwanafunzi wake alisimama upande wangu ili niweze kuifanya kazi hii vizuri. Kila wakati hakuchoka kunishauri na kuniongoza katika kuhakikisha namaliza kazi hii kwa muda uliopangwa, Mungu ambariki sana.

Tatu, nawashukuru wahadhiri wote katika idara ya Lugha na Taaluma za Fasihi ambao walifundisha masomo kwa weledi mkubwa katika ngazi hii ya uzamili. Kwa sababu mawazo yao yamenisaidia sana katika ukamilishaji wa tasnifu hii, miongoni mwao ni Dkt. Zelda Elisifa, Dkt. Nasra Habibu, Dkt. Nestory Ligembe, Dkt. Mohamed Manguo na Dkt. Dunlop Ochieng. Pia napenda kuwashukuru wanafunzi wenzangu tulioshirikiana wakati wote wa masomo yetu hususani katika mijadala mbalimbali ya kitaaluma.  Mungu awabariki sana.

Mwisho shukrani zangu za dhati ziwaendee wazazi wangu wapendwa; baba yangu Bw. Regnard Yohannes Mbunda na mama yangu Bi Daria Damas Nchimbi. Halikadhalika, kwa dada zangu Mariam Regnard Mbunda na Veronika Regnard Mbunda. Bila kuwasahau wadogo zangu Nelson Regnard Mbunda na Ibrahim Regnard Mbunda. Aidha, familia yangu, watoto wangu Francis Elvis Mbunda na Everlyne Elvis Mbunda kwa kuniunga mkono na kunionyesha uvumilivu mkubwa wakati wote wa masomo yangu. Pia nitakuwa mkosefu wa fadhila kama nitawasahau watu wangu wa karibu, Shaaban Sigsberth Ndunguru na Yasin Khalid Ndele.

# IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza vigezo vya utoaji wa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo. Utafiti ulikuwa na malengo mahususi matatu; kubainisha vigezo vinavyotumika kutoa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo, kufafanua maana za kiishara zinazofumbatwa na majina ya watu na kujadili umuhimu wa maana za majina ya watu katika jamii ya Wamatengo. Utafiti huu ulifanyika katika wilaya ya Mbinga Mkoa wa Ruvuma katika maeneo ya Kihangimahuka, Linda, Lukasrasi na Mahande. Mbinu za usomaji makini, usaili na mahojiano ya vikundi zilitumika katika ukusanyaji wa data ambapo data hizo zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa maelezo. Nadharia ya Semiotiki ilitumika katika uchambuzi na uwasilishaji wa data.

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa vigezo vinavyotumika kutoa majina ya watu ni pamoja na tabia au sifa, hisia au imani za wazazi, mazingira na matukio yaliyojiri wakati mtoto anazaliwa. Vigezo vingine ni kazi aliyonayo mtu, maumbile au rangi ya mwili, kipindi mtoto alichozaliwa na mahali alipozaliwa mtoto huyo. Pamoja na vigezo hivyo, imani za dini za wazazi na maendeleo ya sayansi na teknolojia kwa kiasi fulani yameanza kuviathiri vigezo Utafiti umebaini kuwa, majina ya watu yamefumbata maana za kiishara ambazo huakisi historia na maisha ya kila siku katika jamii ya Wamatengo. Pia, maana za majina ya watu zina umuhimu mkubwa katika jamii ya Wamatengo kwa sababu hutambulisha, kuendeleza na kuhifadhi utamaduni wa jamii Wamatengo, kuadibu na kuelimisha jamii.

# YALIYOMO

ITHIBATI ........................................................................................................ i

HAKIMILIKI ..................................................................................................... ii

TAMKO ........................................................................................................... iii

TABARUKU ..................................................................................................... iv

SHUKRANI ....................................................................................................... v

IKISIRI ............................................................................................................ vii

ORODHA YA MAJEDWALI .............................................................................. xii

ORODHA YA VIFUPISHO ................................................................................ xiii

ORODHA YA VIAMBATISHO ........................................................................... xiv

**SURA YA KWANZA .......................................................................................... 1**

**UTANGULIZI WA JUMLA ................................................................................ 1**

1.1 Utangulizi ...................................................................................................... 1

1.2 Usuli wa Mada ............................................................................................... 1

1.3 Tatizo la Utafiti ............................................................................................. 3

1.4 Malengo ya Utafiti ......................................................................................... 4

1.4.1 Lengo Kuu ................................................................................................. 4

1.4.2 Malengo Mahususi ..................................................................................... 4

1.5 Maswali ya Utafiti .......................................................................................... 5

1.6 Umuhimu wa Utafiti ....................................................................................... 5

1.7 Mipaka au Upeo wa Utafiti ............................................................................. 5

1.8 Muundo wa Tasnifu ........................................................................................ 6

1.10 Hitimisho ...................................................................................................... 6

**SURA YA PILI .......... 7**

**MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA .......... 7**

2.1 Utangulizi .......... 7

2.2 Dhana ya Jina .......... 7

2.3 Dhana ya Maana .......... 9

2.4 Tafiti Kuhusu Majina .......... 10

2.5 Pengo la Maarifa .......... 15

2.6 Kiunzi cha Nadharia .......... 16

2.6.1 Nadharia ya Semiotiki .......... 16

2.6.1.1 Mkabala wa Ferdinand Desassure .......... 18

2.6.1.2 Mkabala wa Charles Sander Peirce .......... 19

2.6.2 Mawazo Makuu ya Nadharia .......... 20

2.6.4 Mihimili ya Nadharia ya Semiotiki .......... 21

2.7 Matumizi ya Nadharia ya Utafiti .......... 23

2.8 Hitimisho .......... 24

**SURA YA TATU .......... 25**

**MBINU ZA UTAFITI .......... 25**

3.1 Utangulizi .......... 25

3.2 Mkabala wa Utafiti .......... 25

3.3 Eneo la Utafiti .......... 25

3.4 Walengwa wa Utafiti .......... 26

3.5 Sampuli na Usampulishaji .......... 27

3.5.1 Sampuli .......... 27

3.5.2 Usampulishaji na Mbinu za Usampulishaji .......... 29

3.5.2.1 Mbinu ya Uteuzi wa Madhumuni Maalum ..... 29
3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ..... 30
3.6.1 Njia ya Usomaji Makini ..... 30
3.6.2 Mbinu ya Usaili ..... 31
3.6.3 Mbinu ya Majadiliano ya Vikundi ..... 32
3.6.4 Vifaa vya Kukusanyia Data au Zana za Utafiti ..... 33
3.7 Uchambuzi wa Data ..... 34
3.8 Uzingativu wa Masuala ya Kiitikeli ..... 36
3.8 Hitimisho ..... 39
**SURA YA NNE ..... 40**
**UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ..... 40**
4.1 Utangulizi ..... 40
4.2 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data ..... 40
4.3 Vigezo vya Utoaji Majina ya Watu ..... 41
4.3.1 Majina Yanayotokana na Tabia au Sifa ..... 43
4.3.2 Majina yanayotokana na Hisia za Wazazi au Imani ..... 52
4.3.3 Majina Yanayotokana na Hali au Mazingira ..... 53
4.3.4 Majina Yanayotokana na Kigezo cha Kazi ..... 54
4.3.5 Majina kwa Kigezo cha Matukio ..... 55
4.3.6 Majina kwa Kigezo cha Utamaduni wa Kuendeleza Majina ya Wanyama 57
4.3.7 Majina kwa Kigezo cha Maumbile au Rangi ya Mwili ..... 58
4.3.8 Majina kwa Kigezo cha Wakati au Misimu. ..... 61
4.3.9 Majina kwa Kigezo cha Mahali ..... 62
4.4 Maana za Kiishara Zinazofumbatwa katika Majina ya Watu ..... 63

4.5 Umuhimu wa Maana za Majina ya Watu ........ 68

4.5.1 Kutambulisha Utamaduni wa Jamii ........ 69

4.5.2 Kuhifadhi Historia ya Jamii ........ 69

4.5.3 Kuadibu ........ 69

4.5.4 Kuendeleza Utamaduni wa Utani ........ 70

4.5.5 Kuonesha Hisia ........ 70

4.5.6 Kutofautisha Mtu na Mtu ........ 71

4.5.7 Kuelimisha ........ 71

4.5.8 Kukuza Lugha ........ 72

4.6 Hitimisho ........ 72

**SURA YA TANO ........ 73**

**MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ........ 73**

5.1 Utangulizi ........ 73

5.2. Muhtasari wa Utafiti ........ 73

5.2.1 Vigezo Vinavyotumika Kutoa Majina ........ 74

5.2.2 Maana za Kiishara Zinazofumbatwa katika Majina ........ 74

5.2.3 Umuhimu wa Maana za Majina ........ 75

5.3 Hitimisho ........ 75

5.4 Mapendekezo ya Utafiti ........ 76

**MAREJEO ........ 78**

**VIAMBATANISHO ........ 83**

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 3.1: Jinsi na Idadi ya Watafitiwa ............................................................. 28

Jedwali 4.1: Majina kulingana na Tabia ama Sifa. ............................................... 44

Jedwali 4.2: Majina kulingana na Hisia na Imani za Wazazi................................ 52

Jedwali 4.3 Majina kwa Kigezo cha Hali na Mazingira ...................................... 53

Jedwali 4.4: Majina kwa Kigezo cha Kazi .......................................................... 55

Jedwali 4.5: Majina Yanayotokana na Matukio ................................................... 56

Jedwali 4.6: Majina kwa Kigezo cha Utamaduni wa Majina ya Wanyama........... 58

Jedwali 4.7: Majina kwa Kigezo cha Maumbile au Rangi ya Mwili ..................... 59

Jedwali 4.8: Majina kwa Kigezo cha Wakati/Misimu .......................................... 61

Jedwali 4.9 Majina kwa Kigezo cha Mahali ........................................................ 62

Jedwali 4.10: Majina ya Watu na Maana za Kiishara ............................................. 64

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| Bi | Bibi |
| Bw. | Bwana |
| Dkt | Daktari |
| k.v | kama vile |
| MA | Masters of Arts |
| Na. | Namba |
| n.k | na kadhalika |
| Prof. | Profesa |
| TATAKI | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| Uk. | Ukurasa |

## ORODHA YA VIAMBATISHO

KIAMBATANISHO1: HOJAJI......................................................................…87

KIAMBATISHO2:MASWALI YA USAILI (MAHOJIANO).................................94

KIAMBATANISHO3: RAMANI YA MKOA WA RUVUMA WILAYA YA MBINGA ENEO AMBALO JAMII YA WAMATENGO WANAPATIKANA…..97

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Sura hii inahusu utangulizi wa utafiti unaobainisha na kujadili vipengele vya awali vya utafiti. Vipengele hivyo ni kama vile usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo wa utafiti na mwisho wa sura ni mpangilio wa tasnifu.

## 1.2 Usuli wa Mada

Wataalamu mbalimbali wa isimu jamii wameelezea fasili ya "jina (nomino)". Miongoni mwawataalamu hao ni kama vile Mgullu (1999), Habwe na Karanja(2004) na Matinde (2012) ambao wanaeleza nomino kuwa ni maneno ambayo hutaja watu, vitu au mahali. Hivyo nomino hutajamajina ya watu, vitu, mahali, vyeo, dhana na hata tendo. Katika muktadha huo ndio maana wanaisimuwengine huziita nomino kuwa ni majina.Kihore na wenzake (2009) wanaeleza kuwa jina ni aina ya neno linalotaja au kubainisha viumbehai, vitu visivyo uhai, mahali, hisia, hali, maarifa na tukio katika tungo.Kihore (2009)ametaja aina tatu za majina ambazo ni majina jumuishi, majina ya pekee na majina yakikundi. Pamoja na yote hayo wameeleza kuwepo kwa majina ya kawaida kama vilekiti, daftari, kalamu.

Majina ya pekee ambayo huwa na umbo na tabia ya kipekee au mahususi, majina hayayanaweza kuwa ya watu, mfano, Ahmad, Peter, Khamisi; majina ya mahali, mfano, Mbinga, Mwanza, Tanga, Zanzibar n.k. Ni ukweli usiopingika kwamba Peter ni jina linalowakilisha watu wengi duniani lakini kila mmoja yuko tofauti na mwingine. Hivyo, ni lazima Peter hao watatofautiana kwa rangi, maumbile, kitabia,

mwendo na hatasauti. Hivyo bado litabakia jina la Innocent ni la kipekee kwa kila mmoja.

Hata hivyo, majina hayo ya kipekee, bado kuna majina ambayo hayaleti dhana kuwa jinaalilopewa mtu na wazazi wake baada ya kuzaliwa kuwa ndio tafsiri halisi ya alivyokwa sura, tabia au umbo. Kwa mfano jina “Peter” ambalo alipewa na wazazi wake linalingana na tabia yake? Jina “Peter” kama kiashiria linawiana baina ya mtu anayeitwa hivyo kama ni kiashiriwa cha maana na matendo yake? Kwa muktadha huo, Matinde (ameshatajwa) anasema, kila lugha ina majina ya pekee ambayo hurejeleawatu, siku, miezi, maziwa, mito, miji, vijiji nk. Kwa mfano, Mwita, Mwikali, Wanjala, Dodoma, Marekani, Jumatano, Disemba nk.

Licha ya hivyo, majina hayo huwa hayana uhusiano wa moja kwa moja na kirejelewa chake. Japokuwa mawazo haya yanasigana na yale ya Mutembei (2009) anasaili sababu kwa nini watu hutoa majina ya vitu, mahali, watu au matukio. Mutembei anauliza, Je, ni utambulisho aukielelezo cha yaliyopita au ni utabiri wa yatakayotokea? Akiyajibu maswali hayo, Mutembei (ameshatajwa) anaeleza kuwa, kwa bila shaka kuna msukumounaowafanya watu watoe majina. Majina tunayopewa huwa ni utambulisho wa asilizetu, kwa kumtambulisha mtu, eneo analotoka, tabia na sifa zake na humtofautishamtu mmoja na mwingine. Kwa kuwa lugha inamhusu binadamu, maisha yake, kazizake na jinsi anavyoishi ndani ya mazingira yake (Buberwa, 2010). Kutokuwa na uhusiano wa moja kwa moja wa majina ya pekee ya watu na kirejelewacha jina hilo ndio maana jamii hutoa jina kwa mtu lililowiana naye, jinaambalohushabihiana na umbo au tabia ya mtu huyo baada ya kukulia na tabia fulaniau umbo fulani.

Baadhi ya majina ya watu katika jamii mbalimbali yanaonekana kubeba kwa namna fulaniuhalisia wa jina na kirejelewa yaani mtu aliyepewa jina hilo. Hali hii inatokanana mtu kupewa jina hilo baada ya kutambulika tabia yake. Hivyo, jina analopewa huonesha sifa au tabia ya mtu huyo, au wakati mwingine mtu hupewa jina baada ya kubainika umbilealilonalo ambapo jina hubeba mnasaba wa umbile lake. Majina ya aina hii huwa nitofauti na majina anayopewa mtoto kablaya kujuilikana tabia yake atakayokuwa nayo au umbile lake atakalokuwa nalo baadaye. Aidha, mara nyingi majina yanayotolewa wakati mtoto anapozaliwa huwa ni majina yaurithi au ya ukoo wala hayashabihiani tabia au maumbile atakayokuwa nayo.

Kutokana na hali hiyo, mtafiti amekuwa akijiuliza kwa nini majina ya watu katika jamii ya Wamatengo yanaashiria sifa au hali fulani za kijamii, je majina hayo yanatokea kiholela? Katika kuyatafutia majibu maswali hayo, mtafiti aliona ipo haja ya kuchunguza vigezo vinavyotumika kutoa majina ya watukatika jamii ya Wamatengo ili kubaini maana za kiishara za majina hayo na jinsi yanavyofumbata utamaduni asilia wa jamii hiyo.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Maana za majina ya watu ni eneo ambalo limefanyiwa utafiti na baadhi ya watafiti katika jamii za lugha ya Kibantu. Kwa mfano Ngunga (1995) yeye alichunguza maana kifonolojia na kifonetiki, Kimanga (1994) alijikita katika uchunguzi wa kimofolojia wakati Munyao (2006), Ngunga (1997) na whiteley (1966) wao walijikita katika uchunguzi wa kisintaksia. Vilevile tafiti zingine zilijikita kujadili maana za majina ya watu katika jamii nyingine mfano Wanyoro (Beattie,1957), Wakaguru (Beidelman,1974), Wamburu (Katakami, 1997), Wasukuma (Magesa,

2009), Wahaya (Denice, 2011), Wakamba (Musyimi, 2011), Walulogooli (Olenyo, 2011) na Wayao (Anaphy, 2016). Hata hivyo, hakuna utafiti ambao umeshughulikia vigezo vinavyotumika katika utoaji wa majina ya watu katika lugha ya Kimatengo kwa kuzingatia mtazamo wa kisemantiki ili kuibua maana na ishara ziazofumbatwa na majina ya watu kisemantiki katika lugha ya Kimatengo. Kwa hiyo, tatizo la utafiti huu ni kuchunguza vigezo vinavyotumika katika utoaji wa majina ya watu katika lugha ya Kimatengo ili kubaini maana na ishara za majina hayo katika jamii na jinsi majina hayo yanavyofumbata utamaduni asilia wa jamii hiyo.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una malengo ya aina kuu mbili ambayo ni lengo kuu na malengo mahususi.

### 1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza vigezo vya utoaji wa majina ya watu katika jamii lugha ya Kimatengo ili kubaini maana za kiishara za majina hayo na jinsi yanavyofumbata utamaduni asilia wa jamii hiyo.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

Utafiti huu una malengo mahususi matatu, ambayo ni:

i. Kubainisha vigezo vinavyotumika kutoa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo.
ii. Kufafanua maana za kiishara zinazofumbatwa na majina ya watu katika jamii ya Wamatengo.
iii. Kubaini umuhimu wa maana za majina ya watu katika jamii ya Wamatengo.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i. Vigezo gani vinavyotumika kutoa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo?
ii. Maana gani za kiishara zinazofumbatwa na majina ya watu katika jamii ya Wamatengo?
iii. Je, maana za majina ya watu zina umuhimu gani katika jamii ya Wamatengo?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu mkubwa katika taaluma ya isimu ya Kiswahili hususan semantiki. Kupitia utafiti huu tutachangia maarifa kuhusu vigezo vinavyotumika katika utoaji wa majina, maana na ishara zinazobebwa na majina hayo katika jamii. Hivyo, utafiti huu utatoa mchango wa maarifa katika semantiki ya Kiswahili na Vilevile katika taaluma ya Isimujamii hususan lugha za kibantu kwa ujumla.

Vilevile utafiti huu utaweza kuwa chachu ya tafiti nyingine katika isimu ya lugha. Aidha, mapendekezo ya tafiti zijazo katika maeneo ambayo utafiti huu haukuweza kuyagusa kutokana na malengo mahsusi ya utafiti huu, yatasaidia kuwapa mwongozo watafiti wengine ili kuzalisha tafiti nyingi zaidi.

## 1.7 Mipaka au Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulijikita kuchunguza vigezo vinavyotumika katika kutoa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo ili kubaini maana na ishara zilizofumbatwa na majina hayo. Hivyo, utafiti huu umeshughulikia majina ya watu tu na si vinginevyo. Utafiti

huu haujashughulikia majina ya mahali au vitu, majina yanayotokana na dini ya ukristo ama uislamu. Mfano Musa, Yohana, Yona au Abrahamu, Abdalla, Asha na mengine ya mfano wake.

## 1.8 Muundo wa Tasnifu

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza ni sura tangulizi ambayo inatoa utangulizi wa jumla wa utafiti na kuibua tatizo la utafiti. Sura ya pili inachambua na kujadili mapitio ya maandiko yanayohusiana na utafiti huu na hatimaye kuibua pengo la kimaarifa ambalo ndilo lililohamasisha nia ya kufanya utafiti huu. Aidha, katika sura hii kiunzi cha nadharia kilichoongoza uchunguzi, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti huu kinajadiliwa. Sura ya tatu inafafanua na kujadili mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Sura ya nne ndiyo kiini cha utafiti huu ambapo uchambuzi, uwasilishaji na mjadala wa data na matokeo ya utafiti huu umefanyika kwa kina. Sura ya tano inatoa muhtasari, mapendekezo na hitimisho la utafiti huu.

## 1.10 Hitimisho

Sura hii imetoa utangulizi kwa kubainisha mambo mbalimbali yanayohusiana na utafiti uliofanyika. Mambo hayo ni pamoja na usuli wa tatizo, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasnifu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya kazi tangulizi yanayohusiana na mada ya utafiti. Sura hii ina sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza inahusu maandiko tangulizi na sehemu ya pili inahusu kiunzi cha nadharia. Katika sehemu ya kwanza mjadala umejikita katika vipengele vya dhana ya jina, dhana ya maana, tafiti tangulizi kuhusu majina na pengo la kimaarifa. Sehemu ya pili imeelezea kiunzi cha nadharia ya utafiti iliyoongoza utafiti huu.

## 2.2 Dhana ya Jina

Dhana ya jina imefasiliwa nawataalamu mbalimbali kulingana na mtazamo na mwelekeo wao. Baadhi ya wataalamu hao ni kama vile Kapinga (1983:36) ambaye yeye anafasili jina kuwa ni neno linalotaja kitu fulani kwa lengo la kukitofautisha na kukipambanisha miongoni mwa vitu vingine. Habwe na karanja (2004:8) wanasema jina au nomino ni maneno ambayo hutaja watu, vitu, hali, mahali, vyeo, dhana na hata vitendo. Kwa upande mwingine, BAKIZA (2010:133) wanasema jina ni neno linalotumika kutambulisha mtu, mnyama, kitu, jambo, mahali au vitu. Vilevile Mdee na wenzake (2011:163) wao wanafasili kuhusu jina kuwa ni neno la kumtaja mtu ili kumtofautisha na watu wengine. Aidha, TATAKI (2013:174) jina kuwa ni neno la kumtaja mtu au kitu. Hivyo, kutokana na mjadala huo, tumeona kuwa jina limefafanuliwa kuwa ni neno linalotaja kitu au vitu, wanyama, wadudu, mtu au watu, mahali, jambo na hali hivyo huweza kutofautisha vitu au mnyama au mahali katika muktadha wa sehemu moja na nyingine.

Kwa hiyo, mjadala huu kuhusu dhana ya jina umetusaidia kuweza kufahamu fasili na dhana halisi ya jina na hivyo, katika utafiti wetu ilikuwa rahisi kuelewa tuna maanisha nini tunaposema jina ama majina kwa wingi wake. Hivyo, dhana ya jina imetoa mwanga na kutuongoza katika kubainisha na kupambanua majina ya watu ili kuweza kufikia malengo ya utafiti wetu.

Tunapozungumzia majina ya watu kama wanavyoeleza Msanjila na wenzake (2009:52-53) kwamba kila jamii ina maana ya majina wanayopewa watu wake kutokana na lugha ya jamii yao, maana hizo za majina huwa na uhusiano wa kiutamaduni, umaarufu, majira na matukio muhimu. Mfano jina "Kalyoba" katika Kimatengo lina maana mtu aliyependa sana kuotea jua. Kahweba ni jina la mtu ambalo katika Kimatengo lina maana mtu aliye zaliwa kipindi cha mbayuwayu**.**

Mdee (2010:62-63) anaeleza kwamba: Maana ya majina ya watu ni sifa bainifu za kisemantiki zenye kupambanua neno na kulitofautisha na maneno mengine. Sifa za kisemantiki ni maana ya kiisimu ya neno, na sifa za kitajwa zinazohusu umbile, tabia, matumizi yake kwa jamii inayoongea lugha ile na maana ya kiutamaduni ya kitajwa.

Lyons (1989) na Crystal (1995) wanadai kuwa maana ya majina ya watu ni kiashiria tu cha wale wanaopewa majina hayo. Hivyo, hiki kiashiria ambacho kinakuwa na unasibu katika maana ya majina yanayo rejelewa. Kwa hiyo, kutokana na tafsiri hizi maana ya majina ya watu ni tafsiri zinazo jipambanua katika sifa ya kisemantiki zinazojitofautisha jina moja na jingine, sifa hizo hujitokeza katika mtajwa, umbile, tabia, na maana ya kitamaduni ya jamii hiyo.

## 2.3 Dhana ya Maana

Lyons (1981) anasema kuwa maana ya neno au jina hutokeza pale palipo na kirejelewa chake katika mazingira husika. Obden and Richard (1985) katika kitabu cha "The meaning of the meaning "wameeleza maana ya neno kuwa ni maneno mengine yanayoelezea neno, ama kiashiria cha neno au ishara. Mfano neno Baba hurejelea mzazi wa kiume katika familia.

Kwa upande mwingine, TUKI (1990:39) wanafasili dhana ya maana kuwa ni fahiwa ya neno au kirai kutokana na dhana, matumizi au kitajwa. Lazima kuwepo neno na fafanuzi zake au ufafanuzi wa neno hilo. TATAKI (2013:293) wanasema kuwa maana ni tafsiri ya kitu au jambo, maelezo ya kufanya jambo lieleweke waziwazi, hii ni wazi neno lazima liwe na maana kamili iliyo dhahiri.

Kwa upande wake Resani (2014:109) anasema maana ya maana ni tafsiri anayokuwa nayo msemaji au msikilizaji katika muktadha husika. Hivyo, msemaji ama msikilizaji huweza kuwa na maana juu ya jambo ama kitu fulani kulingana na muktadha na mazingira ya utokeaji ama urejelezi wa jambo hilo. Kwa hiyo, ukichunguza kiujumla wake maana ya maana lazima kuwepo na kitajwa na kirejelewa chake katika muktadha maalum na hivyo huweza kufafanua au kueleza kitu au jambo waziwazi pasipo kuficha.

Ufafanuzi wa dhana ya maana katika utafiti huu umetusaidia kufahamu dhana nzima ya maana. Hii ni kwa sababu maana ndiyo msingi wa utafiti wetu kuhusu majina. Hivyo, uelewa kuhusu dhana ya maana umetuongoza katika kufikia malengo ya utafiti wetu kwa kutusaidia kubaini vigezo vinavyotumika katika utoaji wa majina

katika jamii ya Wamatengo, maana za majina hayo na ishara zinazofumbatwa na majina hayo.

## 2.4 Tafiti Kuhusu Majina

Utafiti kuhusu majina kama tulivyoeleza katika sura ya kwanza, umefanyika kulingana na malengo na mkabala wa tafiti hizo. Hivyo, sehemu hii inajadili kuhusu tafiti hizo na jinsi zinavyohusiana, kufanana na kutofautiana na utafiti huu na pia jinsi zilivyotumika kujenga utafiti huu kinadharia.

Beattie (1957) alichunguza majina ya watu katika Jamii ya Wanyoro wa Uganda na kubaini maana zilizopo katika majina hayo, utafiti wake ulihusisha Jamii ya Wanyoro tu. Kwa ujumla utafiti huo una uhusiano na utafiti wetu ingawa yeye alifanya katika jamii ya Wanyoro waliopo Uganda. Hata hivyo, utafiti huo ni tofauti na utafiti wetu ambao umeangalia vigezo vya utoaji wa majina katika jamii ya Wamatengo. Aidha, matokeo ya utafiti wake yalitusaidia katika kujenga utafiti wetu na hatimaye kufikia malengo ya utafiti huu. Vilevile utafiti wa Beattie ulituongoza katika uteuzi wa nadharia ambayo ilituwezesha kufahamu kuwa majina ya watu jamii ya Wamatengo yana maana gani na vigezo vipi vinavyotumika katika kutoa majina hayo. Hivyo, nadharia ilisaidia katika kutuongoza kuziba pengo jilo la utafiti.

Beidelma (1974) alichunguza majina ya asili ya watu katika jamii ya Wakaguru wa Tanzania na kubaini kuwa majina katika jamii hiyo huwa na maana ndani ya jamii. Hivyo, katika utafiti wake alijishughulisha na majina ya jamii ya Wakaguru tu. Kuna uhusiano kati ya utafiti wa Beidelima na utafiti huu, hii ni kwa sababu tafiti zote zinajihusisha na maana na majina ya watu. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana kwa

sababu utafiti wetu umelenga si kubaini maana tu bali pia kuchunguza vigezo vinavyotumika katika kutoa majina. Tunaamini kuwa vigezo hivyo huambatana na maana, ishara na sababu za kwa nini mtu apewe jina fulani. Hivyo, utafiti huu wa Beidelma umeweza kutusaidia katika ubainishaji wa maana za majina ya watu katika jamii ya Wamatengo na kuwa na upeo katika jamii hiyo tu nakubaini kulikuwa na pengo la kutambua maana za majina katika jamii hiyo.

Mulokozi (1996) ameelezea majina ya mafumbo ambayo hupewa watu katika baadhi ya makabila baada ya kuzaliwa na kaelezea maana ya mafumbo hayo; kwa mfano mtoto anayezaliwa na dosari za maumbile huitwa “njiti”, mtoto anayezaliwa wakati wa njaa huitwa “mwanjaa”na aliyezaliwa wakati wa vita huitwa “mamvita”. Katika kazi yake hiyo Mulokozi hakueleza tathmini ya maana ya majina hayo, ingawaje ameelezea ni kwa vipi majina hayo ya utani hupatikana katika makabila aliyoyaandikia jambo ambalo lilimpa mwanga mtafiti katika kazi yake. Utafiti wa Mulokozi ulitusaidia kuchunguza vigezo vinavyotumika katika kutoa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo. Vilevile, utafiti huo ulitusaidia kwa kutuogoza katika ubainishaji wa maana na ishara zilizofumbatwa na majina ya watu katika jamii ya Wamatengo.

Katami (1997) alichunguza majina asili ya watu katika jamii ya Wambeere wa Kenya na kubaini kuwa majina ya jamii hiyo yana maana. Utafiti wake ulijikita katika kushughulikia majina ya watu katika jamii ya Wambeere tu. Hivyo, utafiti wa Katami ulituongoza katika kuchunguza, kuchambua na kufanya majumuisho ya data zetu kuhusu majina ya Wamatengo. Kwa mantiki hiyo, utafiti wake ulitusaidia kufikia malengo ya utafiti huu ya kuchunguza vigezo vinavyotumika katika utoaji wa

majina kwenye jamii lugha ya Kimatengo na kubaini maana za majina asili ya watu katika jamii hiyo.

Msanjila na wenzake (2009) wametaja umuhimu wa majina katika suala la utambulisho, kwa kueleza uhusiano wa jamii. Majina ya vitu na matukio hutolewa kwa lugha inayozungumzwa na jamii na hubeba maana ambazo kimsingi zinaeleweka na wanajamii. Wametoa mfano wa majina kama vile “Manzale” ni jina la mtoto aliyezaliwa wakati wa njaa, “Matonya” ni mtoto aliyezaliwa wakati wa mvua. Jina la “Chonya Magulu” linatokana na tukio la njaa lililotokea mwaka 1880. Utafiti huu umetusaidia kufikia malengo na majumuisho ya matokeo ya utafiti wetu.

Manyasa (2009) alichunguza majina asili ya watu katika jamii ya Wasukuma wa Tanzania na kubaini kuwa majina hayo yana maana nahivyo alijihusisha na Jamii ya wasukuma tu katika kazi ya Manyasa imetusaidia kutambua kuwa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo yana maana kulingana na tabia na utamaduni wa kupeana majina kama Wasukuma.

Musyini (2011) alichunguza maana za majina asili ya watu katika jamii ya Wakamba wa Kenya ilikubaini maana ya majina hayo. Alijikita katika jamii ya Wakamba tu na alitumia nadharia ya Semiotiki. Utafiti wa Musyini ulifanikishwa vizuri kwa kigezo cha nadharia ya Semiotiki na ikatoa majibu mazuri hivyo mtafiti baada ya kupitia kazi hii ilimsadia kutambua ubora na udhaifu wa nadharia ya Semiotiki katika kuchunguza na kuchambua data kuhusu majina. Hivyo, kupitia mihimili ya nadharia hii tumeweza kufikia malengo ya utafiti wetu.

Denice (2011) alichunguza majina asili katika jamii ya Wahaya Tanzania nakubaini majina hayo yana maana katika jamii husika. Alijikita katika jamii ya Wahaya tu. Kupitia matokeo ya utafiti huu, utafiti huu ulipanua wigo na kuchunguza ni vigezo vipi vinavyotumika katika kutoa majina, maana na ishara zipi zilizofumbatwa na majina hayo. Tofauti na Denice ambaye yeye alichunguza maana za majina tu katika jamii ya Wahaya.

Starks na wenzake (2011) katika utafiti wao wa majina ya utani na utambulisho wa vijana, walibaini kuwa, majina mengi ya utani yanayoibushwa kwa watu katika maisha yao, jina la utani huwa na nguvu ya kimatumizi kwa mhusika binafsi na utambulisho wake. Karibu majina mengi ya utani hubeba sifa za mhusika wa jina na kwa msingi huo jina hilo huibua dhana juu ya mhusika. Dhana hizo huchangia katika kuibua dhana zenye mielekeo mizuri au mibaya kwa mhusika wa jina la utani na mara nyingi huwa sio za kweli.

Olenyo (2011) alichunguza majina asili ya watu ya jamii ya Walulogooli wa Kenya ili kubaini maana za majina hayo. Katika utafiti wakena kwa kutumia nadharia ya Semiotiki aliweza kubaini kuwa majina hayo yana maana katika jamii hiyo. Utafiti huu wa Olenyo ulituongoza na kutusaidia katika utafiti wetu ambapo tuliweza kuchunguza kwa makini maana za majina katika jamii ya Wamatengo na kutumia nadharia ya Semiotiki ilikuziba pengo hili lakuto kutambulika vizuri maana za majina ya watu katika jamii hii ya Wamatengo.

Kuranchie (2012) amefanya utafiti wa majina ya Utani na kuangalia athari za majina hayo kwa wanafunzi katika kujifunza. Katika utafiti wake aligundua kuwa majina ya

15 utani yanatumiwa katika shule nyingi nchini Ghana kama yanavyotumika katika nchi nyingine. Aligundua kuwa karibu asilimia 77.02 ya majina ya utani yanatumiwa na wanafunzi wa elimu ya juu hasa kwa wanaume ingawaje utumiaji huo wa majina ya utani unaathiri muelekeo wao wa kujifunza hasa katika kujaribu kujibu maswali darasani, kutoa maoni yao na kujieleza darasani (Tafsiri yangu).

Ali (2014) alichunguza dhima ya fasili ya majina ya mitaa ya mjini Unguja. Anaeleza kuwa majina ni kipengele kimoja wapo cha fasihi chenye manufaa makubwa kwa jamii ya Ki-Unguja, kwani hutambulisha utamaduni wao, kujua asili yao na kujua siri zilizomo ndani ya majina. Kazi hii imemsaidia mtafiti kuelewa kuwa majina yana siri na manufaa ndani yake hivyo imemshajiisha mtafiti kuchunguza vyema siri hizo katika kufanya tathmini ya maana na vigezo vilivyotumika kupata majina ya utani kwa jamii ya Wapemba. Kihore na Chuwa (1999) walichunguza mbinu za kubuni majina ya kibiashara na wakaona kuwa, kuna mbinu nyingi zinazotumika katika kutoa majina. Miongoni mwa mbinu hizo ni: (i) Kutumia mbinu za kisitiari kwa kufananisha kazi au dhima. Mfano, dawa ya kuulia wadudu waharibifu huitwa komesha, kiboko na hongera. (ii) Kufananisha nguvu, uimara na uwezo. Mfano, saruji chapa mbuni, majani ya chai chapa ya simba. 11 (iii) Kutumia majina ya kijografia. Mfano kibiriti chapa KIBOKO. Kiwanda cha vibiriti aina hii kipo Moshi eneo lililo karibu na kilele cha Kibo cha Mlima Kilimanjaro. Ingawaje mfanano huu wa kisitiari umelenga katika mlima wa Kibo lakini inawezekana pia kufananisha aina hiyo ya kibiriti na mnyama “kiboko”. Kazi yao imesaidia kuelewa maana ya majina na vigezo vinavyopelekea kupatikana kwake.

Kwa upande wa Anaphy (2016) alitumia nadharia ya Semiotiki katika kuchunguza majina asili ya watu katika jamii ya Wayao waishio nchini Tanzania. Matokeo ya utafiti wake yamethibitisha kuwa majina ya jamii hiyo yana maana ambayo hubebwa na majina hayo. Hii ina maana kwamba, majina ya watu huwa hayatolewi kiholela bali hubeba maana maalumu. Hivyo utafiti huu una uhusiano wa kiukamilishano na utafiti wa Anaphy kwa sababu utafiti wake umekuwa chachu ya utafiti huu katika jamii ya Wamatengo na pia utafiti wake umetusaidia katika kukamilisha utafiti huu baada ya kugundua kuwa kuna pengo ambalo linahitaji kufanyiwa utafiti katika jamii ya Wamatengo ili kuona vigezo vinavyotumika katika kutoa majina na pia kubaini maana na ishara zinazojitokeza katika majina ya watu kwenye jamii ya Wamatengo.

Kwa ujumla mapitio ya tafiti tangulizi yanadhihirisha kuwa kuna haja ya kufanya tafiti ili kuweza kuona maana na ishara zinazobebwa na majina katika jamii mablimbali. Aidha, vigezo vya utaoji wa majina vinahitaji kufanyiwa utafiti ili kuweza kuziba pengo hilo.

## 2.5 Pengo la Maarifa

Kama tulivyoona katika mjadala hapo juu, tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu majina katika jamii mbalimbali na kwa kutumia mwelekeo, nadharia na mikabala tofauti. Hata hivyo, kwa upeo wa mtafiti wa utafiti huu, bado hatujapata uthibitisho wa kazi ya utafiti ambayo imechunguza vigezo vya utoaji wa majina katika jamii ya Wamatengo wenye lengo la kubaini maana na ishara za majina hayo katika jamii ya Wamatengo. Hivyo, utafiti uliona hilo ndio pengo ambalo lilihitaji kuzibwa ili kuongeza maarifa juu ya vigezo vya utaoaji wa majina maana na ishara zinazofumbatwa na majina hayo.

Hivyo basi, utafiti huu umejaribu kuziba pengo hilo kwa kuchunguza vigezo vinavyotumika katika utoaji wa majina katika jamii ya Wamatengo ili kubaini maana na ishara zinazofumbatwa na majina hayo ndani ya jamii ya Wamatengo.

## 2.6 Kiunzi cha Nadharia

Kiunzi cha nadharia ni kielelezo cha mfumo wakinadharia kinachomwongoza mtafiti na kumpa mwelekeo katika kuchambua na kuchanganua data za utafiti. Zipo nadharia mbalimbali za semantiki ambazo zingeweza kutumika katika utafiti kama huu, lakini utafiti huu umetumia nadharia ya Semiotiki ili kuweza kuchunguza, kuchambua na kuwasilisha data za utafiti huu. Uteuzi wa nadharia hii ulitokana na kupitia kazi na tafiti mbalimbali zilizofanyika kuhusu majina na ambazo zimetumia nadharia hii na kuona kuwa ni nadharia faafu katika utafiti wa aina hii.

### 2.6.1 Nadharia ya Semiotiki

Nadharia hii iliasisiwa na mwanaisimu wa Ki-swizi Ferdinard de Saussure ambaye aliwekea misingi yake mwaka 1906. Baada ya kifochake 1913, wanafunzi wake Charless Bally na Albert Schehaye waliyaweka mawazo yake pamoja na wakayachapisha katika kitabu kilichoitwa *“Course in General Linguistics”*katika mwaka wa 1916.

Nadharia hii iliendelezwa na mwanafalsafa wa ki-marekani Charles Pierce (1977) na mhakiki Barthes (1977) ambapo walikuwa na mtazamo tofauti na Ferdinard de Saussure. Mtazamo wa Semiotiki uliohusiana na Ferdnard de Saussure ulijikita maana iliyopo dhahiri au maana msingi ya ishara bila kuingilia maana batini ya ishara husika. Watalamu hawa wanahusisha ishara na maana msingi na pia maana

batini kwa kutegemea mantiki. Utafiti huu ulizingatia sana mtazamo wa watalamu hawa ilikupata maana ya majina jamii ya Wamatengo.

Massamba (2004) anaeleza kuwa Semiotiki ni taaluma ya kisayansi inayoshughulikia uchambuzi na uchunguzi wa mifumo ya ishara mbalimbali ikiwa ikizingatia zaidi uhusiano baina ya kiwakilishi na kitajwa. Neno Semiotiki limetokana na neno la kigiriki "semeiotikos" lenye maana ya ubainifu wa ishara ambalo linatokana na neno "semeiotikos" lenye maana ya ishara au alama likitumiwa kwa mara ya kwanza katka Kiingereza na Henry stubbes, *http://www.utwente.ni/cw/theories of semiotics.*

Ferdinand de Saussure kama alivyo nukuliwa na Morri (1971) anafasili Semiotiki ni uhusiano wa alama na kitu, jambo au hali ya kitu inayowakilisha na alama ni kiashiria na kitu ni kiashiriwa. Hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kiashiria na kiashiriwa bali uhusiano huo upo wa kinasibu.

Mtaalamu Nazarova (1996) anafasili Semiotiki ni nadharia inayohusu mfumo wa alama katika mawasiliano kati ya alama na kitu husika. Taaluma hii ya Semiotiki inafafanuliwa kwa alama tatu, ishara ya usababisho mfano mbwa anapobweka sana mawindoni ni ishara ya mnyama yupo karibu, vilevile alama ya miguu inawakilisha mtu kapita. Vilevile, ishara ya mfananisho kiashiria kufananisha kipicha ya ishara na kinachoashiriwa. Mfano picha ya mtu mume katika milango ya choo au mchoro wa kitu na kitu chenyewe. Mfano mwingine michoro ya barabarani, kona kali, kituo cha mabasi pia bendera huwakilisha chama.

Pia, ishara nasibu, katika ishara hizi hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya ishara na kitu kinachoashiriwa lakini ueleweka wake unatokana tu na mazoea tu kwa

kusema uhusiano huu wa kiada kwani haufuati kanuni yoyote. Alama hizo kimsingi ni maneno ya lugha ambayo kimsingi yanaweza kuandikwa au kutamkwa tu. Kwa mfano, jina la mtu inaeleweka ishara hizo zipo katika lugha kiasi kikubwa ingawa katika ufananisho na usababisho zipo pia.

#### 2.6.1.1 Mkabala wa Ferdinand Desassure


Kwa mjibu wa desassure anasema ishara zote ni nasibu yaani hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya ishara na maana yake. Chandler (2002:16) amebainisha kuwa desassaure aliasisi muundo wa sehemu mbili za ishara kwamba ishara imeundwa na:

(i) Kiashiria(signifier) yaani umbo ambalo ishara inachukua

(ii) Kiashiriwa (signfied) ni dhana ambayo ishara inaiwasilisha.

Aidha Ferdinand desassure (1966:67) anaeleza kuwa uhusiano baina kiashiria na kiashiriwa ni wa kinasibu. Mchoro ufuatao ni muundo wa Ferdinand desassure wa ishara umebainishwa katika sehemu mbili kama alivyo ubaini chandler hapo chini.

**MCHORO "A"**




**Chanzo: Chandler (2002:16)**

Maelezo haya yanabainisha kuwa ishara ni nasibu hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya umbo la ishara na maana inayowakilisha umbo hilo. Mfano neno “meza” hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya kitu meza na kitu halisia lakini uhusiano huo umejengwa kinasibu tu.

### 2.6.1.2 Mkabala wa Charles Sander Peirce

Anasema ishara si nasibu lazima iwe na kitu halisia na kitu kinacho kiashiria. Sander peirce hakukubaliana na mtazamo wa Ferdinand de sassure wa unasibu. Peirce aligawa ishara katika sehemu kuu tatu:


(i) Kiashiria (sign vehicle) yaani umbo ishara

(ii) Kiashiriwa (sense) yaani dhana inayopatikana na ishara

(iii) (iii) Kirejeleo (referent) yaani kitu ambacho ishara inakirejelea.

Rejea mchoro wa Charles sander peirce hapo chini kama ulivyo bainishwa na chandler.

**MCHORO “B”**




**Chanzo: Chandler (2002:25)**

Hakubaliani na Ferdinand de Sassure ishara si nasibu bali kuwa kuna kitajwa na kirejeleo chake katika mazingira halisi. Mfano kipima joto ni ishara ya joto kwamba lazima kihusishe na joto. Kata chuma ishara hii lazima ihusishe na chuma, anaendelea kusema ishara hujengwa na vitu vitatu kiashiria, kiashiriwa na kirejeleo katika viwili vya mwanzoni yaani kiashiria na kiashiriwa Sander peirce anapatana na de sassure na Sander peirce anasema lazima mwisho kuwepo na kiashiriwa au kirejelewa.

### 2.6.2 Mawazo Makuu ya Nadharia

Mawazo makuu ya nadharia yamejikita katika sehemu kuu tatu ambazo ni *ishara, kiashiria na kiashiriwa*. Mfumo huu wa ishara ulitumika kuongoza utafiti huu kama ifuatavyo.

(i) Ishara ni dhana ya kuwakilisha au kuashiria kitu fulani mfano “kalyoba”ishara ya aina hii alipewa mtu katika jamii ya wamatengo.

(ii) Kiashiria ni wazo au picha inayojengeka katika akilini mwamsikilizaji kutegemea na utamaduni maalum kuhusiana na jina Fulani lilolisikia au fasiriwa kwake. Mfano “kahosu” limefasiliwa kuwa mtu asiyenakipato chochote (masikini) katika jamii ya Wamatengo.

(iii) Kiashiriwa ni dhana inayorejelewa uhalisiwa wa utamaduni wa jamii maalum. Mfano “Nkere”ni neon linalorejelea mtu mwenye rangi nyeupe ya ngozi yake ya mwili katika utamaduni wa jamii ya wamatengo.

Maana hizi za ishara haitofautiani na ishara yenyewe bali jinsi jamii inavyozitumia na umuhimu unaohusishwa na kiashiria na kiashiriwa. Misingi hii mitatu ya ishara iliwekewa misingi uchanganuzi wa majina ya watu wajamii ya matengo.

### 2.6.4Mihimili ya Nadharia ya Semiotiki

Kwakufafanua zaidi matumizi ya nadharia hii mhakiki Barthes (1977) aliwekea nadharia hii msingi kwa kuonesha nguzo kuu zifuatazo:

(i) Msimbo wa matukio

(ii) Msimbo wa kihemenitiki

(iii) Msimbo wa kisemu

(iv) Msimbo wa Ki-shara

(v) Msimbo wa kirejelezi

Nguzo hizi ni muhimu katika kufasili maana zilizomo kwenye majina ya watu. Aidha zinavyo ingiliana na kuchangiana ziliweza kutumiwa ifuatavyo:

**(i) Msimbo wa matukio**

Tukio ni jambo lililofanyika au tokea.Msimbo huu ulisaidia kwa mtafiti katika kuhakiki matukio ya kiutamaduni katika jamii ya wamatengo yaliyotokea kwa majina husika ya watu mfano tukio la kuwepo kipindi cha njaa kubwa, katika tukio hilo mtoto aliyezaliwa katika kipindi hicho jamii ya wamatengo walimuita “Kanzala”

(ii) **Msimbo wa kihemenitiki**

Misimbo huu ulimsaidia mtafiti kuchunguza fasri ya dhana za majina kwa wapokezi wa jamii. Mfano mama alificha mimba baadaye akajifungua mtoto kwa siri mtoto

huyo alipozaliwa alipewa jina “Ngamanyika”maana hajulikani kwa jamii ya wamatengo.

**(iii) Msimbo wa kisemu**

Neno “semu” hutumika kuzielezea sifa bainifu za kisemantiki sifa hizi zinazotuwezesha kupata picha fulani katika kazi kwa kuibua fahiwa za maana. Msimbo huu ulimwezesha mtafiti kufafanua picha zamaana za majina ya watu jamii ya wamatengo zinazojengwa katika akilini mwawatu kutegemea utamaduni wa wamatengo. Mfano neon “kayola” jina hili linajenga sifa mbaya yakutopendwa na watu katika tamaduni ya wamatengo. Jina hilo hupewa mtu au mtoto huashiria mtu au mtoto huyo hawezi kaa sehemu moja bila kuondoka.

**(iv) Msimbo wa Ki-ishara**

Ishara huwakilisha viashiliwa fulani, uhusiano kati ya ishara na kiashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni. Msimbo huu ulimsaidia mtafiti katika kutathmini viwakirishi na viwakilishwa vya maana katika jamii ya Wamatengo. Kwa mfano jina “kapulisa” humaanisha mtu mwongo, mtu huyo maranyingi huongea uongo katika jamii ya wamatengo. Msimbo huu ulimsaidia sana mtafiti kuchanganua majina yenyesifa mbalimbali katika jamii ya wamatengo.

**(v) Msimbo wa Kirejelezi**

Urejelezi huu huunda uhalisia mahususi kutokana na matumizi ya vitufulani vinavyorejelewa na wasomaji kwanjia hiyo kuipa kazifulani nguzo za kitamaduni. Kiashiriwa kinaweza kuwa kilekile balikinacho rejelewa tofauti kwa mjibu wa utamaduni. Msimbo huu ulimsaidia mtafiti kutathimini jinsi upokeaji wa majina na

jamii ya wamatengo wanavyofasiri maana na ishara zinazoambatana na majina hayo. Mfano jina "kalema" linamaana mtu anayeishi milimani au maana nyingine mtu anayelima hekali nyingi za mazao tofauti.

Hivyo, mihimili mitano ya nadharia imemsaidia mtafiti kuweza kuchunguza, kukusanya na kuchambua data za maana ya majina katika jamiii ya wamatengo na kubaini fahiwa zilizopo katika majina hayo.

**2.7 Matumizi ya Nadharia ya Utafiti**

Utafiti huu umetumia mikabala yote miwili ya nadharia ya Semiotiki katika chunguzi, uchambuzi, ufasili na uwasilishaji wa data za utafiti huu. Nadharia ya Semiotiki imesisitiza zaidi katika katika ishara na hivyo kuonesha kiashiria na kiashiriwa cha umbo la ishara na maana ya ishara. Nadharia hii iliuongoza utafiti huu katika kubainisha maana za majina asili ya watu wa jamii ya Wamatengo na hivyo kudhihirisha kuwa majina ni sehemu ya ishara za maneno ambayo yana maana (ishara za maneno rejelewa)

Aidha, utafiti huu ulitumia nadharia ya Semiotiki na mikabala yote miwili ili kukidhi na kukamlisha malengo ya utafiti huu. Kwa kuwa mikabala yote miwili ya nadharia ya Semiotiki inarejelea kitu kimoja katika muktadha uleule ili kusaidia ubaini maana ya kile kinacho rejelewa.

Mtafiti aliamua kutumia nadharia ya Semiotiki katika utafiti huu badala ya nadharia nyinginezo. Mtafiti aliona nadharia hii inafaa sana katika kuwezesha kubaini maana za majina ya watu kwa sababu inahusisha moja kwa moja kiwakilishi na kiwakilishwa kulingana na mihimili ya nadharia husika na kupata maana ya kitu

(kitajwa na kirejelea chake). Hivyo, mtafiti ameweza kupata matokeo chanya kutambua majina ya jamii ya Wamatengo na kubaini kitajwa au jina lenyewe na kirejelea maana (kisemantiki) iliyobebwa katika jina hilo.

## 2.8 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amefanikisha kuonesha sehemu alizo pitia, mapitio ya kazi kuhusiana na mada ya utafiti, mapitio ya kazi tangulizi za watafiti wengine zinazo husiana na mada ya utafiti. Vilevile ameweza kufafanua nadharia ya utafiti aliyotumia katika kupata maana ya majina ya watu katika jamii ya Wamatengo waishio mkoani Ruvuma Mbinga ndani ya nchi ya Tanzania.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inajadili mikabala, mbinu na vifaa vilivyotumika katika utafiti huu. Kwa ujumla, utafiti huu umetumia mkabala wa kitakwimu na usio wa kitakwimu katika kukusanya, kuzichambua, kuziwasilisha na kuzijadili data za utafiti huu. Jilala (2014: 89) akimnukuu Spicer (2012) anasema utafiti wa kitakwimu na usio wa kitakwimu hujazilizana na kukamilishana (taz. pia Creswel, 2009; Silverman, 2010). Kwa hiyo, utafiti huu ulihusisha mbinu za utafiti wa kitakwimu na usio wa kitakwimu katika misingi ya ukamilishano na ujazilizano. Kwa ujumla, sura hii inajadili yafuatayo: eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, utafiti tangulizi, mbinu za ukusanyaji data, uthabiti na kuaminika kwa uchambuzi wa data na hitimisho.

## 3.2 Mkabala wa Utafiti

Utafiti huu umetumia mkabala wa kimaelezo katika uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti. Enon (1999) anasema data za utafiti ni taarifa ambazo zinakusanywa, kuchunguzwa na kufanyiwa makusudio ya kuchanganuliwa ili kutoa matokeo halisia ya utafiti. Katika utafiti huu, mbinu ya mkabala wa kimaelezo ilitumika katika kukusanya na kuwasilisha data za utafiti. Sababu ya kutumia mkabala wa kimaelezo imezingatia malengo ya utafiti huu ambayo yanahitaji ufafanuzi na maelezo zaidi kuliko data za kitakwimu.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni mahali maalumu ambapo data za utafiti hukusanywa (taz. Polit na Hungler,1999). Hivyo data za utafiti huu zilikusanywa katika eneo la Wilaya ya

Mbinga mkoani Ruvuma nchini Tanzania. Wilaya ya Mbinga ni wilaya ambayo wakazi wake ni kabila la Wamatengo ambao kulingana na malengo ya utafiti wetu ndiyo walengwa wakuuWamatengo. Aidha katika wilaya hiyo data zilikusanywa katika kata za; Kihangimahuka katika Kijiji cha kijij Kihangimahuka, kata ya Linda katika kijiji cha Linda, Kata ya Lukarasi katika kijiji cha Lukarasi na kata ya Utiri kijiji cha Mahande.

Sababu kuu ya kuchagua kufanya utafiti katika kata hizo ni kwamba ndizo kata ambazo wakazi wake wazawa ni kabila la Wamatengo na hutumia lugha ya Kimatengo katika mawasiliano ya kila siku. Hivyo kulingana na malengo ya utafiti huu ambayo ni kuchunguza maana za majina ya watu katika kabila la Wamatengo tuliona kuwa maeneo haya yanafaa kutupatia data toshelevu zinaweza kukidhi malengo ya utafiti huu. Vilevile, sehemu hizi hupitika kwa urahisi kutokana kuwepo kwa barabara nzuri na mawasiliano. Mbinu iliyotumika kuchagua eneo hilo ni mbinu ya usambulishaji nasibu na lengwa ilikupata sampuli.

### 3.4 Walengwa wa Utafiti

Kwa mujibu wa Spata (2003), na Komba na Tromp (2006), sampuli ni jumla ya wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi wakiwemo wanyama, vitu na matukio ambayo mtafiti amekusudia kuyahusisha katika kukusanya data za utafiti wake. Vilevile kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao mtafiti amewakusudia na ambao kutoka kwao atapata taarifa anazozihitaji katika utafiti wake (Kombo na Tromp, 2006; Enon, 1998). Kwa hiyo, walengwa wa utafiti walikuwa ni watu wa kabila la Wamatengo.

Utafiti huu ulilenga watu ambao ni wa jamii ya Wamatengo, wanaopatikana katika wilaya ya Mbinga. Hivyo, mtafiti alitumia walengwa watu wazima kuanzia miaka 45 mpaka 80. Sababu ya kuchagua kundi hili ni kwamba tuliamini kuwa watu hao ni wajuzi na wamilisi wa lugha ya Kimatengo. Vile vile kundi hilo lina umahiri zaidi wa asili ya lugha na maana za maneno hususani majina katika lugha ya Kimatengo ukilinganisha na watu wa umri wa chini ya huo ambao wanaweza kuwa hawana ufahamu mkubwa kuhusu asili ya lugha, maneno na maana za maneno katika lugha. Hivyo, ilikuwa rahisi kuwatumia watu wenye umri huo ili kupata data toshelevu na zenye kuaminika. Hivyo, walengwa hawa walimsaidia mtafiti kupata data za msingi ambazo zilisaidia kuchunguza maana zilizopo kaika majina ya watu wa jamii ya Wamatengo.

### 3.5 Sampuli na Usampulishaji

Enon (1998), Spata (2003), Bryman (2004) na Walliman (2011), wanaeleza kuwa usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu kutoka kundi lengwa ili litumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwa kuwa sio rahisi kutafiti kundilengwa zima. Zipo mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa katika uteuzi wa sampuli, lakini sampuli ya utafifi huu imetumia mbinu moja ambayo ni mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalum.

#### 3.5.1 Sampuli

Sampuli ni sehemu ya walengwa wa utafiti iliyo teuliwa Kushiriki katika utafiti ikiwakilisha kundi lengwa la utafiti. Lobiondo - wood na Haber (1998). Mtafiti alilazimika kuteua kikundi kidogo cha watu ambao waliowakilisha jamii nzima ya Wamatengo ilikupata data za utafiti (kupata maana za majina ya asili jamii ya

Wamatengo). Mtafiti alitumia jinsia zote na idadi ya watu kulingana na kila kata na kijiji. Watu wazima umri 45-80 ambapo mwenye umri wa miaka kati ya 40-80. Kwa mujibu wa Mdee na wenzie (2013:378) ni mtu mzima.

Kwa mujibu wa Spata (2003), na Komba na Tromp (2006), sampuli ni jumla ya wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi wakiwemo wanyama, vitu na matukio ambayo mtafiti amekusudia kuyahusisha katika kukusanya data za utafiti wake. Vilevile, kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao mtafiti amekusudia na ambao kutoka kwao atapata taarifa anazozihitaji katika utafiti wake (Kombo na Tromp 2006 ; Enon 1998). Kwa hiyo, walengwa wa utafiti walikuwa kama kielelezo kinavyo onesha jedwali hapo chini:

**Jedwali 3.1**: Jinsi na Idadi ya Watafitiwa

| **KATA** | **KIJIJI** | **KUNDI** | **JINSIA** | |
|---|---|---|---|---|
| | | | **WANAUME** | **WANAWAKE** |
| LUKARAS | LUKARAS | WATU WAZIMA | 17 | 12 |
| UTIRI | MAHANDE | WATU WAZIMA | 20 | 10 |
| KIHANGI MAHUKA | KIHANGI MAHUKA | WATU WAZIMA | 14 | 11 |
| LINDA | LINDA | WATU WAZIMA | 20 | 12 |
| **JUMLA** | | | **71** | **45** |

**Chanzo: Data za Utafiti**

### 3.5.2 Usampulishaji na Mbinu za Usampulishaji

Enon (1998), Spata (2003), Bryman (2004) na Walliman (2011), wanaeleza kuwa usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu kutoka kundi lengwa ili litumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwa kuwa sio rahisi kutafiti kundilengwa zima. Zipo mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa katika uteuzi wa sampuli, lakini sampuli ya utafifi huu ilitumia mbinu moja ya usampulishaji katika kupata data. Njia ya usampulishaji wa madhumuni maalumu ilitumika.

#### 3.5.2.1 Mbinu ya Uteuzi wa Madhumuni Maalum

Uteuzi wa sampuli kwa kutumia kigezo cha madhumuni maalumu ni uteuzi wa sampuli kwa kuzingatia sababu mahususi. Katika mbinu hii ya uteuzi wenye madhumuni maalum, sampuli huteuliwa kwa kuzingatia vigezo maalum ambavyo vitakuwa na uhusiano na maswali ya utafiti ili yaweze kujibiwa kwa urahisi na ukamilifu (Powell na Conway, 2004). Kombo na Tromp (2006), wanasema, ni uteuzi ambao mtafiti kwa makusudi hulenga kuteua kundi la watu ambao anaamini kuwa ni raslimali anayoitegemea katika utafiti wake. Mbinu hii humpa mtafiti uhuru katika kuteua sampuli itakayowezesha kujibu maswali ya utafiti (Neuman, 2006).

Mbinu ya uteuzi wenye madhumuni maalumu ilitumika kuteua watu wazima. Hivyo, kwa wao kuwa watu wazima waliaminika kuwa wana umahiri juu ya maana za majina, ishara za majina, historia na vigezo vya utoaji wa majina ya watu.

### 3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data katika utafiti huu ulifanywa kwa kutumia mbinu tatu ambazo ni mbinu ya Mapitio ya Maandiko, Usaili, na Majadiliano ya Vikundi. Zipo aina mbili za data, data za msingi au awali na data za upili. Data za msingi ni zile zinazo kusanywa kwa mara ya kwanza na huwa ni mpya. Kothari (2008) anasema ni data ambazo hazijawahi kukusanywa na mtu yeyote kwa minajili ya utafiti kama unavyokusudiwa kufanywa.

Data za upili ni data ambazo zimesha kusanywa na zipo katika maandishi. Kothari (2008) anasema data za upili ni aina ya data katika utafiti wowote ule wa kitaaluma ambazo hukusanywa kutoka katika maandishi na machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti. Utafiti ulitumia njia ya usomaji makini, usaili na majadiliano ya vikundi ili kupata data tosherevu katika utafiti huu.

Utafiti huu ulitumia mbinu zaidi ya moja kwa sababu tuliamini kuwa mbinu hizo zitatusaidia kupata data tosherevu. Aidha, mbinu hizi zilitumika kwa kukamilishana ili kuhakikisha tunapata data za kutosha kwa ajili ya malengo ya utafiti huu.

#### 3.6.1 Njia ya Usomaji Makini

Kwa mjibu wa Bailey (1994) anasema njia ya kupitia uchambuzi wa nyaraka ambazo zina taarifa kuhusu jambo linalotakiwa kutafitiwa. Enon (1998) anasema ni njia inayo husiana na kusoma kwa uangalifu nyaraka zilizoandikwa kama vitabu, magazeti, encyclopidia. Hii ni njia za kupata data za upili. Utafiti utatumia mbinu ya maktaba ilikupata data zaidi ya mada husika na Vilevile kuangalia zaidi namna

watafiti wengine walivyo fanikisha tafiti mbalimbali na mtafiti aweze kuziba pengo lililobaki.

Utafiti umepitia na kusoma machapisho mbalimbali kama majarida, vitabu, kamusi, Encyclopidia, na machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada husika ya utafiti ambayo yanayohusiana na maana za majina asili ya watu Jamii ya Wamatengo waishio nchini Tanzania, Mkoani Ruvuma Wilaya ya Mbinga, njia hii mtafiti alitumia kusoma au kupitia tafiti za watafiti wengine na majarida ambayo yanaendana na kazi ya utafiti husika na hivyo ilisaidia kupata data za upili ya utafiti husika.

Hata hivyo, mbinu hii ilionekana kuwa haiwezi kutupa data za kutosha kwa sababu utafiti huu unahusisha majina ya watu wa jamii mahususi. Hivyo, tuliona kuna haja ya kujua zaidi kuhusu majina kutoka kwa walengwa ambao ni wana jamii ya Wamatengo wenyewe.

Kwa hiyo, utafiti huu uliamua kutumia mbinu ya usaili ili kujibu maswali ambayo msanii alijiuliza katika ukusanyaji wa data kwenye matini. Sehemu inayofuata inajadili kwa kina zaidi kuhusu mbinu ya usaili na namna ilivyotumika katika utafiti huu ili kupata data zaidi kuhusu majina na kwa lengo la kukidhi matakwa ya malengo ya utafiti huu.

### 3.6.2 Mbinu ya Usaili

Usaili ni mbinu ya kukusanyia data ambayo huhusisha mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na mtafitiwa (Kothari, (2013). Katika utafiti huu, mbinu hii ilitumika kuwahoji wahojiwa ambao ni wamilisi wa lugha ya kimatengo. Kundi hili

lilijumuisha watu wazima umri kuanzia miaka 45-80 ili kuweza kupata data zaidi zilizowezesha maswali ya utafiti kujibiwa na hivyo kukamilisha malengo ya utafiti huu. Mtafiti aliandaa maswali kadhaa ambayo yalimwongoza katika kufanya usaili. Uteuzi wa kutumia mbinu hii katika utafiti huu ilitokana na sababu kwamba, ni mbinu ambayo itatusaidia kupata maelezo ya ziada na ufafanuzi wa ziada kuhusu majina, vigezo, maana na ishara zinazofumbatwa na majina ya wamatengo. Hii ilitokana na ukweli kuwa, mbinu hii inatoa uhuru kwa mtafitiwa kujieleza kwa mapana zaidi na vilevile inaruhusu kufafanua yale yasiyoeleweka vema kwa watafitiwa na kuweza kurekebisha majibu kwa kadri ya uhitaji wa mtafiti. Kupitia mbinu hii tulipata kubaini vigezo vinavyotumika katika utoaji wa majina, kupata ufafanuzi wa maana za majina na ishara zilizofumbatwa na majina hayo.

Hata hivyo, pamoja kwamba mbinu hii ilitumika kujaziliza data zilizopatikana katika mbinu ya usomaji wa machapisho tuliona kuwa bado tulihitaji kupata data zaidi. Kwa hiyo, mbinu iliyoonekana kufaa ni mbinu ya majadiliano ya vikundi ambayo tuliamini kupitia mijadala hiyo tunaweza kupata data za kutosha kwa sababu mbinu hiyo humpa uwezo mtafitiwa wa kujadili na kujieleza kuhusu kile kinachojadiliwa. Kwa hiyo sehemu ifuatayo inajadili kwa kina kuhusu mbinu ya majadiliano ya vikundi na jinsi ilivyotumika katika utafiti huu.

### 3.6.3 Mbinu ya Majadiliano ya Vikundi

Mbinu hii ni mbinu ambayo mwongozo wa majadiliano yanafanywa baina ya kundi la watu kati ya sita hadi kumi ambao huwa na sifa na uzoefu unaofanana (Grbich, 1999). Jilala (2008) anasema kuwa majadiliano ya vikundi chini ya msimamizi mmoja yanaongozwa kiasi kwamba ingawa washiriki wanahamasishwa

kuwa huru katika majadiliano lakini lazima kuwepo na mambo ya msingi yanayojadiliwa. Kwa hiyo, msimamizi wa majadiliano hujikita katika mambo mahususi. Mbinu hii ni bora kwa sababu inampa mtafiti taarifa nyingi haraka na kwa muda mfupi. Vile vile ni mbinu muafaka katika kuibua imani, mawazo, maoni na mtazamo ndani ya jamii. Aidha, kwa kutumia mbinu hii wahojiwa katika makundi yao huweza kubadilishana uzoefu kuhusu jambo hilo. Kwa hiyo, sababu ya kutumia mbinu ni kwamba tuliamini kuwa ni mbinu ambayo inaweza kutupatia data nyingi kwa muda mfupi. Aidha, kupitia majadiliano ya wahojiwa tutaweza kupata data za kutosha ili kukidhi malengo ya utafiti wetu.

Kwa kutimia mbinu ya majadiliano ya vikundi, tuliwagawa watafitiwa katika makundi ya watu watano kwa kila kundi. Mjadala wa makundi hayo ulifanyika kwa siku mbili ambapo kila siku kulikuwa na mjadala wa makundi mawili ambayo yalifanya mjadala kwa muda tofauti. Kwa kila kundi mtafiti alifanya majadiliano ya dakika thelathini hadi dakika arobaini. Katika majadiliano hayo mtafiti alilenga kupata maoni, mitazamo na mielekeo juu ya maana za majina, ishara za majina na vigezo vinavyotumika katika utoaji wa majina. Kwa ujumla mbinu hii ilitusaidia kupata data kama ambavyo tulikusudia katika utafiti huu.

### 3.6.4 Vifaa vya Kukusanyia Data au Zana za Utafiti

Kothari (1990) na Dawson (2002) wameeleza vifaa vya kukusanyia data ni kama zana atumiazo mtafiti ilikukusanya data. Vifaa hivi vilimwezesha mtafiti kukusanya data husika na kupata taarifa sahihi za utafiti wake. Katika utafiti huu, data zilikusanywa kwa kutumia vifaa mbalimbali. Vifaa hivyo ni hivi vifuatavyo:

Mtafiti alitumia vifaa vifuatavyo ilikukusanya data zake vizuri katika eneo husika, Daftari, kompyuta, kinasa sauti, kalamu na Biki.

**(i) Daftari**

Hili lilitumika kwa ajili ya kuandikia taarifa mbalimbali za utafiti huu ili kuzihifadhi katika maandishi. Daftari hili lilitumika wakati wa ukusanyaji wa data ili kuzihifadhi, na pia wakati wa uchanganuzi kwa mapitio na marejeleo ya data hizo.

**(ii) Kompyuta**

Kifaa hiki kilitumika kwa ajili ya kuchapisha maelezo yote yanayohusiana na utafiti huu, kuyahifadhi pamoja na kukusanya data kutoka katika mitandao ya tovuti mbalimbali.

**(iii) Kinasa sauti**

Kifaa hiki kilitumika kwa ajili ya kunasa maelezo ya watafitiwa yanayohusiana na utafiti huu na kuyahifadhi kwa ajili ya kumbukumbu ya baadaye wakati wa uchambuzi wa data.

## 3.7 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data kwa mujibu wa Kothari (2013), ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Wakiunga mkono hoja hii Bagdan na Biklen (1992), wakinukuliwa na Omari (2011), wanaeleza kuwa, hii ni hatua muhimu sana katika kutafuta majibu ya tatizo la utafiti husika. Kwa mujibu wa Magigi (2012), anasema uchambuzi wa data ni mchakato wa kukusanya, kuainisha na kupanga data. Katika http://www.businessdictionary (2016) unasema kuwa ni mchakato wa kutathmini

data kwa kutumia sababu za kiuchambuzi na kimantiki kwa kuangalia kila kipengele cha data zilizokusanywa. Zipo mbinu mbalimbali za uchambuzi wa data lakini data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya Uchambuzi wa Kimaudhui na kuwasilishwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo.

Kombo na Tromp (2006), wanaeleza kuwa mbinu ya uchambuzi kimaudhui ni mbinu ambayo huziweka mada kulingana na jinsi zinavyofanana na kuhusiana. Dhana kuu au dhamira kuu hubainishwa na kuwekwa pamoja. Utafiti huu uliitumia mbinu hii kukusanya majina ya watu katika jamii ya Wamatengo ili kukidhi malengo mahususi ya utafiti huu. Sababu ya kuitumia mbinu hii ni kwamba, mbinu hii ni mbinu ambayo imekuwa ikitumiwa na watafiti wengi na hata tafiti nyingi za sayansi ya jamii hutumia mbinu hii. Aidha, tuliamini kuwa mbinu hii itatuwezesha kuzibaini na kuzitenga data zinazohusiana katika kundi moja na kusaidia uchambuzi na mjadala wa data hizo.

Wakati wa kukusanya data za utafiti huu, mtafiti aliandaa daftari au shajara maalum kwa ajili ya kudondoa data za utafiti huu. Kwa kutumia mbinu ya uchambuzi, maudhui mtafiti aliweka na kuzipanga katika kundi moja data zilizofanana na kuhusiana. Kwa mfano, majina yaliyotolewa kwa kigezo kimoja yaliwekwa katika kundi moja. Kwa kufanya hivi, ilisaidia kuchambua na kujadili data za utafiti kulingana malengo mahususi na maswali ya utafiti. Vile vile ilisaidia kurahisisha zoezi la ulinganishaji na ulinganuzi. Mbinu hii ilionekana kufaa zaidi katika kuchambua data za utafiti na kurahisisha uelewekaji wake kwa msomaji kwani iliwezesha kuzipanga na kuzifafanua data hizo na hivyo kuleta maana kwa data na kuwezesha mawazo ya jumla kubainika kulingana na malengo ya utafiti.

Aidha, Williman (2011), anasema data huchambuliwa katika mikabala ya aina mbili, mkabala wa kiidadi na usio wa kiidadi. Mkabala wa kiidadi ni mbinu ya kuchambua data ambazo hutumia nambari kurekodi taarifa na kuchambua kwa kutumia mbinu za kitakwimu.

Katika utafiti huu data zilizopatikana, zilichambuliwa kwa mkabala usio wa kiidadi. Mkabala usio wa kiidadi kwa mujibu wa Tayla na Gibbs (2010) ni mfululizo wa michakato na taratibu zinazotumika katika data za kimaelezo ambazo zimekusanywa katika maelezo, ufahamu au tafsiri za watu na hali zinazotafitiwa.

Enon (1998) ameeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi ni mbinu ya kuchambua data ambayo Mtafiti ametumia mbinu hizi za kimaelezo na uwingi idadi ilikuchambua data za utafiti, mbinu ya uwingi idadi imetumika kuonesha idadi ya walengwa na mbinu ya kimaelezo imetumika kufafanua data za majina ya watu jamii ya Wamatengo na maana zake. Vile vile, utafiti huu umetumia majedwali katika kuwasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti huu.

### 3.8 Uzingativu wa Masuala ya Kiitikeli

Hiki ni kipengele kinachohusika na masuala ya kimaadili katika utafiti na namna mtafiti alivyoweza kuyazingatia kabla ya utafiti, wakati na baada ya kukusanya data. Padgett (2002), anafafanua masuala ya kimaadili ambayo huweza kuibuka na yanayopaswa kuzingatiwa katika aina zote za utafiti. Masuala hayo ni pamoja na kuomba idhini na ruhusa ya kufanya utafiti katika maeneo ya utafiti, usiri, uwazi, ushiriki wa hiari kwa wahojiwa, utiifu na uvumilivu.

Utafiti huu ulihusisha watu kutoka asasi mbalimbali. Kwa vile kila asasi ina sheria, taratibu, kanuni na utamaduni wake, kabla ya kufanya utafiti, mtafiti alipata kibali cha kufanya utafiti kutoka Chuo Kikuu Huria. Kibali hicho kilimsaidia mtafiti kuingia katika maeneo ya utafiti. Kabla ya kuwaona watafitiwa, mtafiti aliwaona viongozi au watu wenye mamlaka katika maeneo husika, ili kujitambulisha na kuhalalisha uwepo wake na kubainisha shughuli alizokusudia kuzifanya akiwa katika eneo hilo husika.

Schutt (2006), anaeleza kuwa ni muhimu sana washiriki wa utafiti wakashiriki kwa kujitolea bila kulazimishwa. Katika utafiti huu, mtafiti aliwaomba washiriki wake kushiriki kwa hiari na kwa kujitolea katika kutoa data za utafiti huu. Wahojiwa walioshiriki katika kutoa data za utafiti huu, walitoa data hizo kwa hiari na kwa uamuzi wao bila kushinikizwa na mtafiti. Wakati wa utafiti, mtafiti aliwaeleza watafitiwa lengo la utafiti na kwa nini anahitaji kupata data hizo, na kisha kuwaomba washiriki kikamilifu katika usaili na kujibu maswali yaliyopo kwa hiari. Hata hivyo, mtafiti alijadiliana kwanza na wahojiwa kuhusu lengo kuu la utafiti huu na matarajio yake ili kupata mawazo, maoni na mtazamo wao. Wahojiwa waliweza kutoa mawazo yao, maoni na mtazamo wao kwa kile wanachokifahamu kuhusiana na lengo kuu la utafiti huu kwa uhuru zaidi. Hii ilisaidia kurahisisha zoezi zima la utafiti na shughuli ya ukusanyaji wa data za utafiti huu.

Utafiti huu ulihusisha zana mbalimbali za kukusanyia data kama vile; simu ambayo ilitumika katika mawasiliano na wahojiwa na kurekodi mazungumzo kati ya mtafiti na wahojiwa. kwa hiyo, kabla ya kutumia zana hiyo, mtafiti aliomba na kuheshimu ridhaa ya washiriki. Mtafiti aliwaeleza wahojiwa sababu na umuhimu wa kutumia

zana hizi na kuwaomba ridhaa ya kuzitumia. Wahojiwa walikubali na kuwa tayari kusailiwa kwa kutumia simu na kurekodiwa katika kinasa sauti cha simu hiyo. Ufafanuzi na uwazi huu ulisaidia katika kukusanya data na kufanya zoezi hilo kuwa rahisi. Data za usaili za utafiti huu zilihifadhiwa katika kinasasauti na kurejelewa pale mtafiti anapohitaji. Speziale na Carpenter (2006), wanaeleza kuwa data za utafiti za usaili zinaweza kuhifadhiwa katika vitu mbalimbali kama vile kinasasauti, maandishi, tepurekoda, picha za video, na picha. Hivyo, vitu vyote vyenye uwezo wa kumtambulisha mhojiwa lazima vihifadhiwe kwa uangalifu wakati wa ukusanyaji wa data mpaka mwishoni mwa utafiti.

Usiri ni jambo jingine la kimaadili ambalo mtafiti alilizingatia wakati wa kukusanya data. Speziale na Ronet, kama walivyonukuliwa na Malangwa (2010), wanasema kwamba washiriki hawanabudi kuhakikishiwa na watafiti kuwa usiri wa data wanazozitoa utazingatiwa. Hii ni pamoja na kuwahakikishia kuwa, data hizo hazitatumika vinginevyo zaidi ya kutimiza malengo ya utafiti huu na bila kubainisha chanzo cha data hizo.

Mtafiti alizingatia pia suala la usiri kwa kuwaahidi na kuwahakikishia washiriki wa utafiti huu, ambao walishiriki katika usaili kuwa, data walizozitoa zitakuwa ni siri ya mtafiti na mhojiwa na zitatumika kwa ajili ya malengo ya utafiti huu. Kwa kuwathibitishia hayo, wahojiwa hawakutakiwa kutaja majina yao, ili kulinda siri ya mtoa data. Vilevile, katika mjadala wa matokeo haya, hakuna urejelezi wa jina uliofanywa katika uchambuzi, uwasilishaji na mjadala wa data. Kulingana na ahadi ambayo mtafiti aliitoa kwa wahojiwa wake, data zote alizokusanya kutokana na usaili kwa kinasa sauti zimehifadhiwa kwa usiri mkubwa. Hii ni kwamba, mtafiti

alichukua tahadhari kubwa katika kuzingatia vipengele vyote vya maadili katika utafiti.

### 3.8 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amejikita zaidi na mbinu mbalimbali za utafiti zilizotumika katika upangaji wa utafiti, kukusanya na kuchambua data. Data hizo zitajibu maswali ya utafiti, na matokeo yake ndiyo yatatimiza malengo ya utafiti huu . Mbinu za usampulishaji iliyotumika ni moja yaani; mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalum . Sura hii pia imebainisha na kujadili mbinu zilizotumika kukusanya data za utafiti huu ambazo ni; mbinu ya maktaba, usaili na majadiliano ya vikundi. Baada ya kujadili mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu, sura inayofata inawasilisha, kuchambua na kujadili data na matokeo ya utafiti huu.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji wa data, uchambuzi na mjadala wa matokeo ya utafiti. Aidha, ufafanuzi wa matokeo wa utafiti kuhusu vigezo vya utoaji na maana za majina ya watu katika jamii ya Wamatengo umebainisha data zillizopatikana zimekidhi haja ya lengo la utafiti na madhumuni ya utafiti. Uchambuzi wa data hizo uliongozwa na nadharia ya Semiotiki ambayo mtafiti aliiteua.

## 4.2 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data

Uwasilishaji wa data ni namna ya kupanga data katika mtiririko maalumu ili ziweze kutoa taarifa vizuri. Uchambuzi wa data ni kuchunguza kwa undani data zilizopangwa na kuzitolea hitimisho, Kombo na Tromp (2006) wanaeleza kuwa uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangailia data zilizokusanywa vizuri kwa namna ambayo inawezeshwa kukamilisha malengo ya utafiti husika(Babble, 1999).

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza vigezo vinavyotumika katika utoaji wa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo ili kubaini maana na ishara za majina hayo na jinsi yanavyofumbata utamaduni asilia wa jamii hiyo. Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi matatu. Lengo la kwanza lilitaka kubainisha vigezo vinavyotumika kutoa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo, lengo la pili lilihusu kufafanua maana za kiishara zinazofumbatwa na majina ya watu katika jamii ya Wamatengo, na lengo la tatu lilikuwa ni kufafanua umuhimu wa maana za majina ya watu katika jamii ya Wamatengo.

Ili kufikia malengo hayo, utafiti huu ulitumia mbinu ya usomaji makini kwa kufanya mapitio ya maandiko kwa kusoma, kuchunguza na kuchambua majina ya watu. Hivyo basi, kwa kutumia mbinu hiyo, utafiti huu uliweza kubainisha majina ya watu katika jamii ya Wamatengo. Aidha, utafiti huu ulitumia mbinu za usaili na majadiliano ya vikundi ili kujaliza na kufafanua zaidi data za utafiti huu.

Vilevile, data zilizokusanywa kwa mbinu ya usomaji makini, usaili na majadiliano ya vikundi zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa maudhui. Kwa kutumia mbinu hii mtafiti aliandaa mwongozo wa kuchambulia data ambapo matini zinazofanana ziliwekwa pamoja ili kurahisha uchambuzi na uwasilishaji wake. Sehemu ifuatayo inawasilisha, kuchambua na kufafanua data na matokeo ya utafiti kwa mujibu wa malengo mahususi ya utafiti.

## 4.3 Vigezo vya Utoaji Majina ya Watu

Sehemu hii inahusu uchambuzi wa data za lengo mahususi la kwanza la utafiti huu ambalo lilitaka kubainisha vigezo vinavyotumika kutoa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo. Data za lengo hili zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usoamji makini kutoka katika mapitio ya maandiko mbalimbali, mbinu ya usaili na majadiliano ya vikundi ambapo watu wazima wa jinsia zote mbili walishirikishwa kutoa data zinazolenga kukidhi lengo hili. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa jamii ya Wamatengo hutoa majina ya watu kwa kuzingatia vigezo maalumu ambavyo ni sehemu ya utamaduni, mila na desturi za Wamatengo. Wakati wa usaili na majadiliano ya vikundi, wahojiwa wa utafiti huu walibainisha vigezo vinavyotumika katika utoaji wa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo kuwa ni:

i. Tabia au sifa aliyonayo mtu
ii. Hisia za wazazi na imani katika jamii
iii. Mazingira
iv. Matukio ambayo yaliyotokea wakati mtoto anazaliwa
v. Kazi aliyonayo mtu
vi. Maumbile au rangi ya mwili
vii. Wakati mtoto anazaliwa
viii. Mahali.

**Chanzo:** Data za utafiti (2020)

Kupitia data hizo ambazo zilitolewa na wahojiwa wakati wa usaili na majadiliano ya vikundi, data hizo zinadhihirisha kuwa majina ya Wamatengo hayatolewi kiholela bali huzingatia vigezo kama ambavyo vimebainishwa hapo juu. Vigezo vilivyotajwa na wahojiwa vinadhihirisha wazi kuwa majina ya Wamatengo hutolewa kwa kuzingatia utamaduni wa jamii hiyo kulingana na mazingira na maisha ya jamii hiyo.

Aidha, pamoja na uzingativu wa vigezo hivyo, matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa jukumu la kumpa mtoto wa Kimatengo jina hufanywa na wazazi na anayetoa jina la mtoto ni baba. Jina hili hutolewa wakati mtoto anapozaliwa na wakati mwingine akishakuwa mkubwa hupewa jina kulingana na matakwa ya wazazi. Baada ya imani za dini ya Kiislamu na Kikristo kuingia katika jamii ya Wamatengo, mtoto anapozaliwa hupewa jina la asili na pia baada ya hapo hupewa jina la dini kulingana na imani ya wazazi wake ama imani yake binafsi anapokuwa mkubwa. Hii inadhihirisha kuwa Wamatengo huwa na majina ya asili na majina ya dini.

Aidha, jamii ya Wamatengo huwapa watoto majina ambayo huwa na maana kama ilivyo kwa jamii nyingi za Kiafrika. Mbiti (1991) anaeleza kuwa majina ya watu ni sehemu muhimu katika utamaduni wa Waafrika. Kila jina huwa na maana yake ambayo wanapewa watoto wazaliwao katika jamii za Waafrika, hivyo maana hiyo huchukuliwa kuwa na uzito mkubwa.

Sehemu ifuatayo inajadili jinsi vigezo vya utoaji wa majina vinavyotumika katika kutoa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo.

### 4.3.1 Majina Yanayotokana na Tabia au Sifa

Jamii ya Wamatengo huwapatia wanajamii au watoto wao majina yanayotokana na tabia au sifa za wazazi wao walizozionyesha mara baada ya kuzaliwa. Mengi ya majina hayo ni ya lakabu. Mulokozi (1996:42) anaeleza kuwa lakabu ni majina ambayo hupewa baadhi ya watu kulingana na sifa zao za mwili, za kinasaba kitabia na kimatendo. Katika jamii, majina haya mara nyingi huonesha sifa au tabia nzuri ama mbaya alizonazo mtu aliyepewa jina husika kulingana na jinsia yake. Tuangalie mifano katika jedwali namba 4.1 kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.1**: Majina kulingana na Tabia ama Sifa.

| NA. | JINA | JINSIA | MAANA |
|---|---|---|---|
| 1 | Kambanga | Mwanaume | Mtu anayependa kuiba au kukwapua vitu vya watu. |
| 2 | Kakongobi | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kujiona yeye ni mwanaume (Kidume) au mwenye mamlaka ya amri ya vitu vyote katika familia. |
| 3 | Kanyama | Mwanaume | Mtu anayependa kula nyama zaidi au mlafi wa nyama kuliko mboga za majani. |
| 4 | Kamuliku | Mwanaume | Mtu anayependa kumulikia moto mara nyingi wakati wa usiku. |
| 5 | Kaweba | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kubadilika badilika kama mbayuwayu. |
| 6 | Kanyelela | Mwanaume | Mtu anayependa kunywa sana pombe |
| 7 | Kigonera | Mwanaume au Mwanamke | Mtu anayependa kulala sana wakati wa mchana na usiku. |
| 8 | Kipyega | Mwanamke | Mwanamke anayeapenda kupika ugali mgumu. |
| 9 | Kasembi | Mwanamke | Mtu anayependa sana kula ndege. |
| 10 | Kaborakambi | Mwanaume au Mwanamke | Mtu mwenye tabia ya kulala kila sehemu. |
| 11 | Kakuri | Mwanaume | Mwanaume anayependa kula panya au mtu mwenye tabia kama panya |
| 12 | Kaselenge | Mwanamke | Mwanamke mwenye tabia ya umbea |
| 13 | Kulatura | Mwananamke au mwanaume | Mtu anayependa kukopa kopa au muongo. |
| 14 | Kaselu | Mwanamke au Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kuchelewa chelewa kwa kila jambo (mchelewaji). |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 15 | Kanima | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kigeugeu cha mambo. |
| 16 | Lunyengu | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kutembea tembea bila faida. |
| 17 | Kandindi | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kuruka ruka au mtu mwizi. |
| 18 | Kahimba | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kuwa na hasira waakati wote. |
| 19 | Kajunzu | Mwanaume | Mtu anayependa kuachia nywele bila kunyoa. |
| 20 | Kaholola | Mwanaume | Mtu mwenye tabia kupenda kuokoteza mazao shambani mwawatu baada ya kuvuna. |
| 21 | Kanzeba | Mwanaume | Mtu mwenye tabia kuruka ruka kama njiwa yaani hatulii nyumbani. |
| 22 | Kijemi | Mwanaume au Mwanamke | Mtu anayependa kusimama bila kukaa chini mara nyingi. |
| 23 | Kajuni | Mwanaume | Mtu anayependa kula ndege mara nyingi. |
| 24 | Kapulasengi | Mwanamke au Mwanaume | Mtu mweanye tabia ya kupenda kuongea uongo. |
| 25 | Kanzara | Mwanamke au Mwanaume | Mtu anayependa kula |
| 26 | Majebee | Mwanaume au Mwanamke | Mtu anayependa matembezi muda mwingi hakai nyumbani |
| 27 | Kapanza | Mwanaume | Mtu anayependa kunyoa upaa. |
| 28 | Ngomalitako | Mwanaume | Mtu mwenye kupenda wanawake zaidi kimapenzi. |
| 29 | Ng’ang’a | Mwanamke au Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kutoelewa mambo (mjinga). |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 30 | Kapenga | Mwanamke au Mwanamke | Mtu mwenye tabia ya kudakia mambo au kupokea wageni mbalimbali. |
| 31 | Makanika | Mwanamke au Mwanamume | Mtu mwenye tabia ya kukataa au kugoma mambo mbalimbali anayoambiwa. |
| 32 | Kandwinya | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kujifanya anaweza mambo yote kumbe mengine hawezi. |
| 33 | Kahosu | Mwanaume | Mtu mwenye hali ya umasikini (hanakipato). |
| 34 | Kapulisa | Mwanaume au Mwanamke | Mtu mwenye tabia ya kusema uongo (hawezi kusema au kuongea ukweli). |
| 35 | Kahuku | Mwanamke au Mwanume | Mtu mwenye tabia ya ubahili katika matumizi fedha au vitu. |
| 36 | Kahupa | Mwanaume | Mtu anayependa kula nyama za mifupa. |
| 37 | Kalobelela | Mwanaume | Mtu anayependa kunywa pombe mpaka kulewa. |
| 38 | Kabotori | Mwanaume | Mtu anayependa kubeba maguduria au madumu ya maji anapoenda kuchota maji. |
| 39 | Lihakanzusi | Mwanaume | Mtu anayependa kula asali au kupakua asali. |
| 40 | Sindukumoso | Mwanaume | Mtu anayependa kutembea na wasichana kimapenzi mara kwa mara. |
| 41 | Nganyatu au Likanyatu | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya matembezi muda wote hatulii nyumbani |
| 42 | Mbalangonde | Mwanaume | Mtu anayependakula ugali na maharage au chakula pamoja na mboga ya maharage. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 43 | Kandeu | Mwanaume | Mtu mwenye tabia yakutonyoa ndevu muda wote. |
| 44 | Linga'nga' | Mwanaume au Mwanamke | Mtu mwenye tabia ya kutoelewa mambo (mjinga). |
| 45 | Kajamanda | Mwanamke au Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kubepa majamanda au vifurushi kwenye harusi mara kwa mara. |
| 46 | Likolo | Mwanaume au Mwanamke | Mtu anayependakula mboga nyingi ugali kidogo |
| 47 | Makandi | Mwanaume | Mtu anayependakula kande mara kwa mara kuliko chakula kingine. |
| 48 | Likungo | Mwanaume | Mtu mwenye kupenda kula likungu au chakula kinachotengenezwa na wadudu wadogo warukao waitwao hununa (wapigao kelele masikioni) |
| 49 | Mpyoli | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kuongea kitu kisicho na maana. |
| 50 | Likesa | Mwanaume | Mtu anayependa kufyeka fyeka nyasi. |
| 51 | Kalyongu | Mwanaume | Mtu anayependakula maboga |
| 52 | Kalombi | Mwanaume au Mwanamke | Mtu anayependakula mahindi mabichi. |
| 53 | Kasulusi | Mwanaume au Mwanamke | Mtu mwenye tabia ya kujizila (litakalotokea lolote lile au vyovyote vile na iwavyo). |
| 54 | Kahipa | Mwanamke au Mwanaume | Mtu anayependa Kula dagaa zaidi. |
| 55 | Kahomba | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kupendelea Kula samaki. |
| 56 | Makenya | Mwanaume | Mtu ambaye miguu yake kwenye nyayo imepasuka makea. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 57 | Kapongo | Mwanaume | Mtu mwenyetabia ya kupenda wanawake kufanyanao mapenzi aumtu mwenye tabia ya kujiona yeye mwanaume mwenye nguvu kuliko wengine. |
| 58 | Punguwane | Mwanaume au Mwanamke | Mtu mwenye hali ya kutokuwa na akili timamu (ana upungufu wa akili) |
| 59 | Limbombombu | Mwanaume au Mwanamke | Mtu ambaye yupo yupo tu (hanaustarabu kimavazi) |
| 60 | Nseja | Mwanaume au Mwanamke | Mtu mwenye hali ya kuwa mzee. |
| 61 | Nzendajika | Mwanaume au Mwanamke | Mtu mwenye tabia ya kutembea peke yake. |
| 62 | Limbomba | Mwanamke au Mwanaume | Mwanaume mwenye tabia ya kuwa na tabia ya kike (umbea) au mwanamke umbo kubwa (mnene). |
| 63 | Makupi | Mwanaume | Mtu anayependakula panya buku. |
| 64 | Ngahyoka | Mwanaume au Mwanamke | Mtu mwenye hali ya kutokuwa na akili timamu (ana upungufu ya akili) |
| 65 | Jwaheho | Mwanaume au Mwanamke | Mtu mwenye tabia ambayo haibadiliki yeye tabia yake ni ileile hatakama ukimshauri. |
| 66 | Limeteki | Mwanaume au Mwanamke | Mtu mwenye tabia ya kutorudi kwake akienda sehemu. |
| 67 | Lwihwa | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kigeukige au kubadilika badilika katika makubaliano waliokusudia. |
| 68 | Mbalakujenda | Mwanaume au Mwanamke | Mtu mwenye tabia ya kutembea sana, hakai nyumbani. |
| 69 | Kango'ngo'teka | Mwanamke au Mwanaume | Mtu mwenye tabia kulaumu au kulalamika muda wote. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 70 | Kamemesela | Mwanamke | Mtu mwenye tabia ya kuongea umbea mara kwa mara. |
| 71 | Kahengaleku | Mwanamke | Mtu mwenye tabia ya kuzuia mambo au vitu au kukataa vitu alivyopewa. |
| 72 | Kahimbi | Mwanamke au Mwanaume | Mtu anayependa kula magimbi. |
| 73 | Kabutuka | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kukimbia kimbia, hawezi kutembea mwendo wakawaida. |
| 74 | Ngalangi | Mwanaume | Mtu anayependakula mahindi ya kukaanga (bisi) |
| 75 | Kanzika | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya ubinafsi (umimi). |
| 76 | Ndemibwaka | Mwanaume au Mwanamke | Mtu mwenye tabia ya uvivu hataki kufanyakazi. |
| 77 | Libambo | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kushona viraka katika nguo yake iliyotoboka au mwanaume mwenye umbo kubwa (mnene) |
| 78 | Kikwinda | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kuchomekea vizuri shati kwenye suruali au mwanaume mwenye tabia ya kufunga taulo bila kuvaa shati. |
| 79 | Kahona | Mwanaume | Mtu anayependa kuvuta tumbaku mara kwa mara. |
| 80 | Katuru | Mwanaume | Mtu anayependa sana kunywa togwa au turu. |
| 81 | Kabundura | Mwanaume | Mtu anayependa kuvaa kaputura muda wote. |
| 82 | Kahabi au Mhabi | Mwanamke au Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kuwa na hali ya uchawi au mchawi. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 83 | Kikwandapai | Mwanaume | Mtu anayependa kusugua chini kwenye ardhi muda wote. |
| 84 | Kapesa | Mwanaume | Mtu anayependakula nyama ya sungura au mtu mwenye tabia ya ujanja ujanja. |
| 85 | Kahinahina au kanekula | Mwanamke | Mwanamke anayependa kucheza ngoma (muziki) |
| 86 | Kalembwani | Mwanaume | Mtu anayependa kulembua macho. |
| 87 | Kabejabeja | Mwanaume au Mwanamke | Mtu anayependa kucheza ngoma (muziki) |
| 88 | Kapahi | Mwanaume | Mtu anayependa kula panzi. |
| 90 | Mkomba | Mwanaume | Mwanaume anayependa kukomba mboga kwenye sufuria au kwenye chungu. |
| 91 | Sumpongu | Mwanaume | Mtu ambaye hapendi kuoa. |
| 92 | Kalimwendu | Mwanaume | Mwanaume mwenye sifa ya kupenda kutembea mwendo wa haraka. |
| 93 | Kasuha | Mwanamke | Mtu anayependa kuloweka mahindi au mihogo kisimani au kwenye ndoo au sufuria. |
| 94 | Kasupuria | Mwanaume | Mtu anayependa kupika vyakula jikoni muda wote. |
| 95 | Kanyeleka | Mwanaume au Mwanamke | Mtu anayependa kunywa pombe sana. |
| 96 | Kajabo | Mwanaume | Mwanaume anayependakula mihogo. |
| 97 | Lihoku | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kuwa na hali ya uzee kati mambo yake anayofanya wakati si mzee. |
| 98 | Kingonza | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kuwa mchafu muda wote. |
| 99 | Lihonzu | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kurukaruka au kutotulia mahali au nyumbani. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 100 | Kinyanyambuli | Mwanaume | Mtu mwenye sifa ya kuwa mkali muda wote ukimuanza au ukibishananaye. |
| 101 | Kajore | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya kukubali mambo mbalimbali bila kuyachambua. |
| 102 | Kangongu | Mwanaume au Mwanamke | Mtu mwenye hali ya kuwa mfupi. |
| 103 | Kapyonda | Mwanaume | Mtu anayependa kubeba au kupakua mizigo kutoka kwenye gari |
| 104 | Kapondu | Mwanaume | Mtu mwenye tabia ya upole muda wote. |
| 105 | Kandwangi | Mwanaume | Mtu mwenye hali ya kutokuwa na akili timamu au mtu mwenye kichwa kikubwa. |
| 106 | Mahengo | Mwanaume | Mtu anayependa sana kufanya kazi za mikono (kulima). |
| 107 | Kapyoga | Mwanaume au Mwanamke | Mtu mwenye tabia ya kutotulia wakati wote yeye hufikiria safari. |
| 108 | Kaponga | Mwanaume | Mwanaume anayependa sana kula wali. |
| 109 | Kisalawile | Mwanaume | Mtu anayependa sana kusalisali. |
| 110 | Kagunila | Mwanaume | Mwanaume anayebeba magunia au kusafirisha magunia. |
| 111 | Kalamba | Mwanaume | Mtu anayependa kuulamba muda wote. |
| 112 | Ponda | Mwanaume | Mtu anayependa kazi ya uhunzi kutengeneza vitu (kuponda vitu) mfano visu,mapanga au fyekeo. |
| 113 | Kasapa | Mwanaume | Mtu anayependa kufua nguo mara kwa mara. |
| 114 | Kasuku | Mwanaume | Mtu anayependakula matunda ya porini ya itwayo masuku. |

**Chanzo: Data za Utafiti, 2020**

Katika data zilizowasilishwa hapo juu zinadhihirisha kuwa watu katika jamii ya Wamatengo hupewa majina kwa sababu ya tabia au sifa walizo nazo wenyewe au wazee wao. Aidha, baadhi ya majina hutumiwa na jinsi zote kama inavyojidhihirisha kwenye jedwali hapo juu. Vilevile, majina hayo hubeba ishara na maana kulingana na tabia ama sifa iliyokusudiwa.

### 4.3.2 Majina yanayotokana na Hisia za Wazazi au Imani

Majina ya watu katika jamii ya Wamatengo hutolewa kwakuzingatia kigezo cha hisia na imani walizonazo wazazi ambazo zilifanya wazazi hao kuwapatia majina watoto wao waliozaliwa na watu waishio katika jamii hiyo.

**Jedwali 4.2:** Majina kulingana na Hisia na Imani za Wazazi

| Na. | JINA | JINSIA | MAANA |
|---|---|---|---|
| 1. | Kanzika | Mwanamke au Mwanaume | Mtu aliyezaliwa au bakia peke yake baada ya wengine kufariki. |
| 2. | Ngamanyika | Mwanamke au mwanaume | Mtu asiyejulikana na wanajamii wengi katika mtaa wao. |
| 3. | Mwahabe nkolongu | Mwanaume au mwanamke | Mtu mwenye imani za kishirikina au mchawi mkubwa. |
| 4. | Alamikuha | Mwanamke au mwanaume | Mtu aliyenusurika kufa katika jamii. |
| 5. | Kasiki | Mwanaume au mwanamke | Mtoto aliyezaliwa njiti au aliyezaliwa kabla ya muda. |
| 6. | Ngayhoha | Mwanamke au mwanaume | Mtu mwenye imaniyakuwa hanahakili timamu katika jamii. |

**Chanzo: Data za Utafiti (2020)**

Data katika jedwali na. 4.2 hapo juu inadhihirisha kuwa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo hutolewa kwa kuzingatia kigezo cha hisia na imani ya jamii ya watu. Wamatengo huwapatia watoto wao au watu katika jamii yao majina ambayo yanayojikita katika hisia na imani walizonazo wanajamii hao.Hali hii huifanya jamii iendeleze baadhi ya majina kutokana na imani na hisia yao,kwa mfano,tunaporejea baadhi ya majina kama jedwali hapo juu tutabaini hali hiyo. Vilevile baadhi ya majina hapo juu yanajitokeza katika jinsi zote. Mfano *Kasiki,* Ngamanyika na *Alamikuha*

### 4.3.3 Majina Yanayotokana na Hali au Mazingira

Baadhi ya watu au watoto katika jamii ya Wamatengo hupewa majina kutoka kwa wazazi wao au kwa wanajamii, kutokana na hali zao na mazingira ambayo jamii hiyo imeyapitia au hali iliyotokea katika jamii kwa mazingira husika.

**Jedwali 4.3** Majina kwa Kigezo cha Hali na Mazingira

| **Na** | **Jina** | **Jinsia** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| 1 | Kahosu | Mwanaume | Mtu mwenye hali ya umasikini au ametokea mazingira ya umasikini katika familia yake. |
| 2 | Kanzika | Mwanaume au Mwanamke | Mtu mwenyeyeishi mazingira ya pekee yake au mbali na wenzake. |
| 3 | Kinunu | Mwanaume | Mtu mwenye hali ya kuwa kimya muda wote. |
| 4 | Kalyoba | Mwanaume | Mtu aliyezaliwa kipindi au mazingira ya jua (kiangazi) |
| 5 | Kawheba | Mwanaume | Mtu aliyezaliwa kipindi Cha mbayuwayu |
| 6 | Kandyondu | Mwanaume | Mtu mwenyehali ya kupenda kutukana. |
| 7 | Kalamba | Mwanaume | Mtu mwenye kupenda kulamba lamba. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8 | Kalabila | Mwanaume | Mtu mwenye kupenda kujihimu Kati mazingira ya asubuhi. |

**Chanzo: Data za utafiti, 2020**

Katika jedwali na. 4.3 hapo juu, data inadhihirisha kuwa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo hutolewa kwa kigezo cha hali au mazingira waliyonayo. Aidha,baadhi ya majina hapa yameonesha kutumika kwa jinsia zote kwa wanaume na wanawake, mengine yametumika kwa wanawake tu au kwa wanaume tu kama jedwali linavyo jidhilisha hapo juu. Pia, maana zinazoambatana na majina hayo hubeba ishara ya hali au mazingira yaliyosababisha kutolewa kwa jina hilo. Mfano, Kalabila ni Mtu mwenye kupenda kujihimu Katika mazingira ya asubuhi, Kinunu ni Mtu mwenye hali ya kuwa kimya muda wote.

### 4.3.4 Majina Yanayotokana na Kigezo cha Kazi

Majina haya ni majina ambayo watu hupewa kutokana na kazi za wazazi au wazee wao katika jamii ya Wamatengo. Aidha, kuna majina ambayo watu wazima hujipa au hupewa majina kulingana na kazi wanazozifanya ama walizokuwa wanazifanya ndani ya jamii.

**Jedwali 4.4:** Majina kwa Kigezo cha Kazi

| **Na** | **Jina** | **Jinsia** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| 1 | Kagunila | Mwanaume | Mtu anayependa kazi ya kubeba magunia au kusafirisha magunia sehemu moja kwenda nyingine au kupakua kwenye gari. |
| 2 | Likesa | Mwanaume | Mtu mwenye kupenda kufanya kazi ya kufyeka. |
| 3 | Mwihe | Mwanaume | Mtu mwenye kazi ya kuiba vitu vya watu wengine. |
| 4 | Mpyoli | Mwanaume | Mtu mwenye kazi ya kuongea uwongo muda wote. |
| 5 | Kasoma | Mwanaume | Mtu anayependa Sana kusoma vitabu |
| 6 | Kalema | Mwanaume | Mtu anayependa kufanya kazi ya kulima. |

**Chanzo: Data za Utafiti, 2020**

Katika jedwali namba 4.4 hapo juu tunaona kuwa majina yaliyotolewa yametokana na kazi za wazazi wao, wazee wao ama kazi anazozifanya mtu mwenyewe katika jamii. Kama ambavyo imeelezwa, wahojiwa walibainisha kuwa baadhi ya watu kulingana na kazi ama majukumu yao ndani ya jamii hujipa ama kupewa majina yanayosadifu kazi wanazofanya. Aidha, majina hapa yameonesha kutumika kwa jinsia ya wanaume tu kama jedwali linavyo jidhilisha hapo juu.

### 4.3.5 Majina kwa Kigezo cha Matukio

Hiki ni kigezo ambacho majina ya watu hutolewa kulingana na matukio ndani ya jamii. Utoaji wa majina huzingatia tukio ambalo limetokea kwa wakati huo ambao mtu amezaliwa ama wakati ambao mtu anajipa ama kupewa jina. Tazama mifano katika jedwali namba 4.5 hapa chini:

**Jedwali 4.5:** Majina Yanayotokana na Matukio

| Na. | Jina | Jinsia | Maana |
|---|---|---|---|
| 1 | Kahundi | Mwanaume | Mtu aliyezaliwa kipindi cha mawingu mazito. |
| 2 | Kapahi | Mwanaume | Mtu aliyezaliwa kipindi cha panzi wengi. |
| 3 | Kalyoba | Mwanaume | Mtu aliyezaliwa kipindi cha jua (kiangazi). |
| 4 | Kahweba | Mwanaume | Mtu aliyezaliwa kipindi cha baridi. |
| 5 | Kahusa | Mwanaume au mwanamke | Mtu aliyezaliwa kipindi cha mavuno. |
| 6 | Malelu | Mwanaume | Mtu aliyezaliwa kipindi cha msiba. |
| 7 | Kambulika | Mwanaume | Mtu aliyezaliwa kipindi cha kumbi kumbi. |
| 8 | Kangondu | Mwanaume | Mtu aliyezaliwa kipindi cha vita. |
| 9 | Ngondumwitu | Mwanaume | Mtu aliyezaliwa kipindi ambacho hakuna Vita. |
| 10 | Kanzala | Mwanaume au mwanamke | Mtu aliyezaliwa kipindi cha njaa. |
| 11 | Kajabo | Mwanaume | Mtu aliyezaliwa kipindi cha mavuno ya mihogo. |
| 12 | Lujendu au kasapwali | Mwanaume au mwanamke | Mtu aliyezaliwa kipindi cha safari , mzazi wake akisafiri. |
| 13 | Kasuku | Mwanaume | Mtu aliyezaliwa kipindi cha masuku. |

**Chanzo: Data za Utafit, 2020**

Mifano katika jedwali namba 4.5 hapo juu inaonesha majina na matukio ambayo husababisha jina hilo kutolewa. Hii ina maana kwamba jamii ya Wamatengo hutoa majina kulingana na matukio ambayo yanajitokeza kwa wakati ambao mtu anazaliwa ama anapewa jina hilo. Mfano jina *Lujendu au kasapwali* hupewa mwanamke ama mwanaume ambaye amezaliwa kipindi cha safari yaani mzazi wake anapokuwa safarini. Aidha, baadhi ya majina hapa yameonesha kutumika kwa jinsia zote kwa

wanaume na wanawake, mengine yametumika kwa wanaume tu kama jedwali linavyo jidhilisha hapo juu.

### 4.3.6 Majina kwa Kigezo cha Utamaduni wa Kuendeleza Majina ya Wanyama

Utafiti huu ulibaini kuwa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo hutolewa kwa kuzingatia kigezo cha Utamaduni, wana utamaduni wa kuwapa watoto wao majina ya ukoo ambayo huendeleza majina ya wanyama mbalimbali. Kigezo kinacho zingatia kurithishwa majina ya ukoo kwa wanajamii. Sababu za kutolewa majina haya ya wanyama katika jamii. kulingana na wahojiwa walisema kutokana na wanajamii wa kwanza katika utamaduni huo kuwa na tabia ya uhusiano au kuwachukia wanyama hao katika mazingira husika, kwa mfano kuwa na uhusiano wa wanyama hao wengi na kutumiwa katika kitoweo, wazawa hawa wa kwanza walipewa majina “komba”, “Mapunda” kwaupande mwingine kuwachukia wanyama hao wazawa wakwanza wautamaduni huu waliwapa majina ya wanyama “Nyoka”, “Kunguru” kuonesha wanyama hawa walikuwa wabaya katika mazingira hayo na hivyo majina ya wazawa hao yaliendelee kurithiwa katika ukoo mpaka siku hizi.

**Jedwali 4.6:** Majina kwa Kigezo cha Utamaduni wa Majina ya Wanyama

| NA. | JINA | JINSIA | MAANA |
|---|---|---|---|
| 1 | Komba | Mwanaume au Mwanamke | Mtu hupewa jina hili la ukoo ilikuendeleza jina la mnyama waporini aitwaye komba. |
| 2 | Mapunda | Mwanaume au Mwanamke | Mtu hupewa jina la ukoo ilikuendeleza jina la mnyama aitwaye punda. |
| 3 | Nyoka | Mwanamke au Mwanaume | Mtu hupewa jina la ukoo ilikuendeleza jina la mnyama aitwaye nyoka. |
| 4 | Makunguru | Mwanaume | Mtu hupewa jina hili katika ukoo ilikuendeleza jina la mnyama kunguru. |

**Chanzo: Data za Utafiti, 2020**

Data katika jedwali na. 4.6 hapo juu linaonesha majina ambayo hupewa mtu yakiwa ni majina ya wanyama. Majina haya hutolewa kwa watu ili kuendeleza ukoo au kurithishwa katika koo na majina hayo hujulikana baadhi ya majina ya wanyama waliokuwa wanauhusiano nao au kutokuwa na uhusiano na wanajamii hao wa kwanza waliopatiwa na vizazi vilivyofuata vilirithitu kulinganana majibu ya wahojiwa. Aidha, majina hapa yameonesha kutumika kwa jinsia zote kwa wanaume na wanawake kama jedwali linavyo jidhilisha hapo juu.

### 4.3.7 Majina kwa Kigezo cha Maumbile au Rangi ya Mwili

Utafiti huu ulibaini kuwa kigezo cha maumbile au rangi ya mwili wa mtu hutumika kutoa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo. Baadhi ya watu katika jamii ya hiyohupewa majina kutokana na maumbile au rangi ya mwili waliyonayo hata hivyo wahojiwa katika utafiti huu walisema majina hayo hupewa watoto kuanzia miaka mitatu na kuendelea. Vilevile, wahojiwa walidai hayatolewi majina hayo watoto

chini ya miaka mitatu ama anapozaliwa tu kwasababu ni vigumu kubaini rangi za mwili halisi ya mtoto kulingana na ukuaji wake kama ni nyeupe au nyeusi. Vilevile, hutolewa majina hayo watu wazima kulingana na maumbile yao ya kimo mfano mfupi sana aliitwa "kajipi" na mrefu sana "Ndasu". Kwaupande wa watu wenye ulemavu wa viungo wakuzaliwa nao au kutokana na ajali walipatiwa majina kulingana na ulemavu wao majina haya ya utani kulingana na utamaduni wa jamii ya wamatengo mfano "Kaboku" mtu aliye na mkono mmoja au "Kagolu" mtu mwenye mguu moja hata kama anatembelea upande mwingine vifaa saidizi. Mtafiti alitafiti jamii kuwa majina hayo hupatiwa wanajamii wote bila kuzingatia jinsia vilevile majina hayo yanaumuhimu wa kuendeleza utani na utamaduni wa jamii husika. Baadhi ya majina hayo ni haya yafuatayo:

**Jedwali 4.7:** Majina kwa Kigezo cha Maumbile au Rangi ya Mwili

| **Na.** | **Jina** | **Jinsia** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| 1 | Kasiki | Mwanamke au mwanaume | Mtu mwenye umbile la ufupi (yeye si mrefu) |
| 2 | Kajipi | Mwanaume au mwanamke | Mtu ambaye ni mfupi zaidi kuliko watu wengine. |
| 3 | Ndasu | Mwanaume au mwanamke | Mtu mwenye umbeli la urefu (mtu mrefu) |
| 4 | Kapehi | Mwanamke au mwanaume | Mtu ambaye ni mwembamba katika umbile lake. |
| 5 | Kajiru | Mwanaume au mwanamke | Mtu mwenye rangi nyeusi katika ngozi yake(mweusi). |
| 6 | Nkere | Mwanaume au mwanamke | Mtu mwenye rangi nyeupe katika ngozi yake (mweupe). |
| 7 | Kakutu | Mwanaume au | Mtu mwenye masikio makubwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | mwanamke | kuliko watu wengine. |
| 8 | Kalihu | Mwanaume au mwanamke | Mtu mwenye jicho moja. |
| 9 | Kagolu | Mwanaume au mwanamke | Mtu mwenye uremavu wa mguu mwenyemguu mmoja. |
| 10 | Katumbu | Mwanaume | Mtu mwenye kitambi. |
| 11 | Likanyatu | Mwanaume | Mtu mwenye miguu mikubwa (akitembea nyayo zake huonyesha kubwa) |
| 12 | Kahingu | Mwanaume au mwanamke | Mtu mwenye shingo ndefu kuliko wengine katika jamii. |
| 13 | Kaboku | Mwanaume au mwanamke | Mtu mwenye uremavu wa mkono yaani ana mkono mmoja. |

**Chanzo: Data za Utafiti (2020)**

Katika Jedwali namba 4.7 hapo juu tunaona majina ambayo hutolewa kwa watu kulingana na maumbile au rangi zao. Aidha baadhi ya majina hapa yameonesha kutumika kwa jinsia zote.

Mtafiti aliuliza ni kwa nini majina haya hutolewa kwa watu wa jinsia zote ili kujua endapo suala la ujinsia linajitokeza katika majina ya Wamatengo. Wahojiwa walieleza kuwa majina hayo yalikuwa yanatolewa kwa jinsia zote kwakuangalia maumbile, rangi na ulemavu walionao wanajamii hao na wahojiwa walidai kuwa majina hayo yalikuwa yanaendeleza utani katika utamaduni wa jamii hiyo ya wamatengo.

### 4.3.8 Majina kwa Kigezo cha Wakati au Misimu.

Kigezo cha wakati ni kigezo ambacho hutumika kutoa majina katika jamii ya Wamatengo. Wazazi wa watoto walitumia kigezo cha wakati au msimu kuwapa majina Watoto wao. Utafiti huu ulibaini baadhi ya majina ya watu ambayo hutolewa kwa kutumia kigezo cha wakati/misimu. Tazama mifano katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.8:** Majina kwa Kigezo cha Wakati/Misimu

| NA | JINA | JINSIA | MAANA |
|---|---|---|---|
| 1 | Kawheba | Mwanaume | Mtu aliyezaliwa kipindi cha mbayu wayu wengi, ukatokea msimu huu |
| 2 | Kalyoba | Mwanaume | Mtu aliyezaliwa kipindi cha jua Kali , kukawa na msimu huu wa ' kalyoba' |
| 3 | Kahosu | Mwanaume | Mtu alipewa jina hilo kipindi hicho (wakati huo) ameishiwa (yaani hana kitu) |
| 4 | Kaywola | Mwanaume | Mtu ambaye hupendelea kunoa visu au mapanga au shoka kipindi Cha kuandaa mashamba. |
| 5 | Kuhoba | Mwanaume | Mtu ambaye kipindi hicho alipotea nyumbani kwao na wakamtafuta akaonekanatena |

**Chanzo: Data za Utafiti, 2020**

Data katika jedwali namba 4.8 hapo juu inaonesha mifano ya majina ambayo hutolewa kwa kuzingatia kigezo cha wakati/misimu. Mifano hiyo inadhihirisha kuwa watu katika jamii ya Wamatengo hupewa majina kwa sababu ya wakati au misimu inayojitokeza. Aidha, data za utafiti huu zimedhihirisha kuwa majina ya watu yanayotolewa kwa kigezo cha wakati/misimu hutolewa kwa watu wa jinsia moja tu ambayo ni ya kiume ambapo majina hayo hayatolewi kwa jinsia ya kike.

Vilevile, utafiti huu ulihoji sababu ya majina ya aina hii kutolewa kwa wanaume tu na si wanawake. Wahojiwa walieleza kuwa majina hayo hupewa wanaume tu kwasababu wao ndio walijihusisha sana katika shughuli za uzalishaji na kutafuta kipato kwa jamii katika utamaduni wa jamii ya wamatengo. Pia, wahojiwa walihusisha kipindi kigumu cha maisha ambacho wanajamii hao walikabiliana nacho hasa wanaume katika kutafuta liziki katika kipindi husika. Mfano “kalyoba” kipindi cha jua kali wanaume walivyo kuwa wakishughulika kulima ilikupata kipato. Majina hapo juu yameonesha kutumika kwa jinsia moja ambayo jinsia ya kiume.

### 4.3.9 Majina kwa Kigezo cha Mahali

Baadhi ya watu au watoto jamii ya Wamatengo walipewa majina kutokana na mahali walipokuwa wakiishi. Baadhi ya majina hayo ni haya yafuatayo:

**Jedwali 4.9** Majina kwa Kigezo cha Mahali

| NA. | JINA | JINSIA | MAANA |
|---|---|---|---|
| 1 | Lihange | Mwanaume | Mtu alipewa jina hilo kutokana anaishi sehemu iitwayo Kihangi |
| 2 | Mbelenga | Mwanaume | Mtu aliyeishi sehemu itwayo Lupilinga, alijipatia jina hilo. |
| 3 | Kalosi | Mwanaume | Mtu alipewa jina hilo kutokana alikuwa anapendelea kuishi jirani na mto. |
| 4 | Kalema | Mwanaume | Mtu alipewa jina hilo kutokana alikuwa anaishi juu ya milima. |
| 5 | Panduhi | Mwanaume | Mtu alipewa jina hilo kwa sababu alikuwa anaishi mazingira machafu yenye takataka nyingi. |

**Chanzo: Data ya Utafiti, 2020**

Katika jedwali hilo,maana za majina ya watu imedhihirisha kuwa watu katika jamii ya Wamatengo hupewa majina kwa sababu ya mahali wanapoishi. Aidha, baadhi ya majina hapa yameonesha kutumika kwa jinsia moja wanaume tu.Wahojiwa walisema majina hayo walipewa wanaume kwasababu wao walikuwa waanzilishi wa kwanza kuishi katika sehemu hizo kabla ya wanajamii wengine na wengine walijipatia waowenyewe wanajamii hao ilikuonesha wao ndio walianza kuishi katika maeneo hayo na kuendeleza shughuli zao za kutafuta kipato Mfano “kalema”jina hili huwakilisha mtu aliyekuwa anaishi kwenye mlima fulani akiendeleza shughuli zake za ufugaji na kilimo. “kalosi’ jina hili mtu alijipatia au kupewa jinsia ya kiume kuwa yeye alikuwa wa kwanza kuishi katika sehemu hiyo jirani na mto akiendeleza shughuli za kiuvuvi na kilimo. Vilevile, mtafiti aliendelea kuwasaili wahojiwa iwapo kila mtu anayeishi maeneo hayo hupewa majina hayo. Walijibu hapana, walidai majina hayo walijipatia au pewa wale waliokuwa waanzilishi tu wa kwanza katika kuishi katika maeneo hayo na kujihusisha na shughuli zao za uvuvi, ufugaji na kilimo hasa jinsia ya kiume kulingana na utamaduni wa jamii hii ya wamatengo na majina hayo yalibeba maana na ishara. Kwa watu waliohamia katika sehemu hiyo hawapewi majina hayo kutokanakuwa wao sio waanzilishi wa kwanza katika maeneo hayo. Hata kama walijishughulisha na shughuli mbalimbali za uzalishaji mali na hayo yalikuwa majibu ya wahojiwa wa jamii ya wamatengo.

### 4.4 Maana za Kiishara Zinazofumbatwa katika Majina ya Watu

Sehemu hii inachambua na kujadili lengo mahususi la pili la utafiti huu ambalo lilikuwa ni kufafanua maana za kiishara zainazofumbatwa na majina katika jamii ya Wamatengo. Wahojiwa kupitia mbinu ya usaili na katika majadiliano ya vikundi

walieleza kuwa majina ya Kimatengo huwa na maana za kiishara ambazo hufumbatwa na majina hayo kulingana na utamaduni na mazingira ya jamii ya Kimatengo. Vilevile, wahojiwa waliweza kubainisha maana za majina waliyopewa katika karatasi. Hivyo, data za utafiti huu zilidhihihirisha kuwa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo hubeba maana za kiishara ndani ya jamii. Aidha, utafiti huu uliabini kuwa upo uhusiano mkubwa baina ya maana za majina na kile kinachorejelewa. Tazama mifano ifauatayo katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.10:** Majina ya Watu na Maana za Kiishara

| **Na.** | **Jina** | **Maana** |
|---|---|---|
| 1 | Kanyama | Mtu anayependa kula nyama mara kwa mara |
| 2 | Kakuri | Mtu anayependa kula panya |
| 3 | Kaholola | Mtu anayependa kuokoteza mazao sehemu ambamo mazao hayo yamevunwa |
| 4 | Kajuni | Mtu mwenye tabia ya kupendelea kula ndege wa porini |
| 5 | Kapanza | Mtu anayependa kunyoa upaa |
| 6 | Kahosu | Mtu mwenye kipato cha chini (masikini) |
| 7 | Mhabe | Mtu mwenye tabia ya imani ya ushirikina |
| 8 | Kanzika | Mtu mwenye kupenda kujitenga pekee yake au kuishi eneo la pekee yake tu hataki kuwa jirani na wenzake |
| 9 | Kalabila | Mtu mwenye tabia ya kjihimu sana katika safari au kazi |
| 10 | Likesa | Mtu mwenye kupenda sana kufyeka nyasi mashambani |
| 11 | Kagunila | Mtu anayejishughulisha shughuli ya kubeba magunia (kuli) |
| 12 | Mwihe | Mtu anayejihusisha na wizi wa vitu |
| 13 | Kalema | Mtu anayependa sana kulima mashamba zaidi ya hekali tano |
| 14 | Malelu | Mtoto aliyezaliwa kipindi cha msiba uliotokea nyumba ya wazazi husika |
| 15 | Kangondu | Mtu anayependa vita mara kwa mara |

| | | |
|---|---|---|
| 16 | Kapahi | Mtu anayependa sana kula panzi au jina hupewa mtoto aliyezaliwa kipindi cha panzi wengi |
| 17 | Kasiki | Mtu mwenye kimo kifupi sana |
| 18 | Nkere | Mtu mwenye rangi nyeupe ngozi ya mwili |
| 19 | Kajiru | Mtu mwenye rangi nyeusi ya ngozi ya mwili |
| 20 | Kapehi | Mtu mwembamba au ambaye hana nguvu |
| 21 | Lihange | Jina la mtu aliyejitatia kuwa yeye mwanzilishi wa kwanza kuishi katika sehemu iitwayo Kihangi |
| 22 | Kalema | Jina la mtu aliyepewa kutokana yeyekuishi sehemu ya mlima peke yake tu |
| 23 | Kalosi | Jina alilojipatia mtu kuwa yeye alikuwa mwanzilishi wa kuishi kalibu na mto wa kwanza katika eneo hilo bila watu wengine kabla kuhamia eneo hilo |
| 24 | Kalyoba | Mtu alipatiwa jina hilo kutokana alizaliwa kipindi cha jua kali au kiangazi |
| 25 | Kahweba | Mtu aliyezaliwa kipindi cha mbayu wayu wengi |
| 26 | Komba | Jina la ukoo au kurithishwa ambalo asiliyake huonesha uhusiano wa aliyepewa lilitokana na wanyama |
| 27 | Mapunda | Jina la ukoo au kurithishwa ambalo asiliyake huonesha uhusiano wa aliyepewa lilitokana na wanyama |
| 28 | Mpyoli | Jina ambaloalipewa mtu kutokana na kupenda kuongea uwongo mara kwa mara katika mazingira husika |
| 29 | Kambanga | Jina ambalohupewa mtu kutokana na tabia yake kupenda kudhulumu au kuchukua vitu vya watu kinguvu |
| 30 | Kunyema | Jina ambalohupewa mtu mwenyetabia ya kupenda kutoroka nyumbani kwakunyatia |

**Chanzo: Data ya Utafiti, 2020**

Katika jedwali hapo juu, wahojiwa walieleza kuwa majina hayo yanamaana mbalimbali katika jamii ya Wamatengo. Maana za majina yaliyomo katika jedwali hapo juu yalifafanuliwa kama ifuatavyo:

Mosi, watu walipewa au kupata majina kutokana na tabia au sifa za wazazi wao au zao wenyewe walizozionesha baada ya kuzaliwa. Kwa mfano, majina yafuatayo: Kanyama, lenye maana ya mtu anayependelea kula nyama mara nyingi. Kakuri, lenye maana ya mtu mwenye kupenda au tabia ya kula panya. Kaholola, lenye maana ya mtu mwenye tabia yakupenda kuokoteza mazao shambani mwa watu.Kajuni, lenye maana ya mtu anayependa kula ndege wa porini naKapanza lenye maana ya mtu anayependa kupenda kunyoa upaa.

Pili, watu walipewa au kupata majina kutokana na hisia walizokuwa nazo wazazi au kwa sababu ya imani ambazo jamii inayo kwa mfano majina yafuatayo: Kanzika linamaana mtu aliyezaliwa peke yake au aliyebakia peke yake wenza wamefaliki waliozaliwa naye. Mhabe, ambalo lina maana ya mtu mwenyeimani za kichawi ambapo Ngahyoka lenye maana ya mtu mwenyehisia hanaakili zote.

Tatu, watu walipewa au kupata majina kutokana na hali waliyonayo au mazingira waliyomo, kwa mfano majina yafuatayo: Kahosu lenye maana ya mtu mwemye haliya kutokuwa na (kitu masikini). Kanzika lenye maana ya mtu anayeishi pekeyake katika mazingira fulani. Kalabila lenye maana ya mtu mwenye kupenda kujihimu au kuwahi mazingira ya asubuhi sana.

Nne, watu walipewa au kupata majina kutokana na kazi walizokuwa wakifanya wazee wao au wao wenyewe, kwa mfano majina yafuatayo: Kagunila, lenye maana ya mtu anayefanya kazi ya kubeba au kupakua magunia kutoka kwenye gari. Likesa, lenye maana ya mtu anayefanya kazi ya kufyeka nyasi mashambani. Kalema, lenye

maana ya mtu mwenye kupenda kazi ya kulima sana. Mwihe lenye maana ya mtu mwenye kufanya kazi ya kuiba au kupenda kuiba.

Tano, watu walipewa au kupata majina kutokana na matukio yaliyojiri wakati huo, kwa mfano majina yafuatayo: Malelu lenye maana ya mtu aliyezaliwa kukiwa na msiba nyumbani kwao. Kangondu, lenye maana ya mtu aliyezaliwa kukiwa na vita katika jamii yao. Kapahi lenye maana ya mtu aliyezaliwa wakati wa panzi wengi. Kanzala lenye maana ya mtu aliyezaliwa kipidi kunatukio la njaa katika jamii yao.

Sita, watu walipewa au kupata majina kutokana na maumbile au rangi ya mwili waliyonayo, kwa mfano majina yafuatayo: Kapehi lenye maana ya mtu mwembamba. Kasiki lenye maana ya mtu mwenyeumbile la ufupi (mfupi) na Nkere lenye maana ya mtu mwenye rangi nyeupe.

Saba, watu walipewa au kupata majina kutokana na mahali walipokuwa wakiishi, kwa mfano majina yafuatayo: Lihange lenye maana ya mtu anayeishi sehemu iitwayo kihangi. Kalema lenye maana ya mtu mwenye kuishi milimani au juu ya milima na Kalosi lenye maana ya mtu anayependa kuishi jirani na mto.

Nane, watu walipewa au kupata majina kutokana na wakati au msimu uliopo, kwa mfano majina yafuatayo: Kalyoba lenye maana ya mtu aliyezaliwa wakati wa jua kali. Kahosu lenye maana ya mtu ambaye hanakitu (masikini) na Kahweba lenye maana ya mtu aliyezaliwa wakati wa mbayu wayu wengi ukatokea msimu huu.

Tisa, watu walipewa au kupata majina kwaajili ya kuendeleza ukoo wao katika jamii ya Wamatengo na hii ni kuendeleza utamaduni wao katika jamii. Majina hayo

huendeleza koo za Kimaatengo na hivyo hayo majina yanaendeleza ukumbukwaji wa wanyama mbalimbali. Kama ya vileKomba jina la ukoo katika baadhi ya jamii za Wamatengo ambalo huwakilisha mnyama wa porini aitwaye komba hupenda kulia lia usiku kwenye miti. Mapunda ni jina la ukoo baadhi ya jamii za Wamatengo ambalo huwakilisha mnyama wa porini aitwaye punda. Nyoka ni jina la ukoo baadhi ya jamii za Wamatengo ambalo huwakilisha mnyama wa porini aitwaye nyoka.Ni dhahiri kuwa, kumekuwa na sababu mbalimbali zilizofanya watu kupewa au kupata majina wanayoitwa.

### 4.5 Umuhimu wa Maana za Majina ya Watu

Sehemu hii inajadili lengo mahususi la tatu la utafiti lilikuwa ni kujadili umuhimu wa maana za majina katika jamii ya Wamatengo. Ifahamike kuwa majina ya watu ni muhimu katika jamii kwani huelezea juu ya mtu mwenyewe, utamaduni na shughuli za kiuchumi. Kila jina huwa na maana kwani huwa linaelezea kumhusu mtu na kinachohusika naye (Sitati, 2007). kama tulivyoona kuwa kila jina linalotolewa hutolewa kwa kigezo maaluumu na hubeba maana za kiishara ndani ya jamii.

Hata hivyo, utafiti huu ulienda mbali zaidi kutaka kujua umuhimu wa maana za majina kwa jamii. Kama jina lina maana fulani, je, maana hiyo ina umuhimu gani kwa jamii? Je, maana za majina katika jamii na utamaduni wa Wamatengo zina umuhimu gani kwa jamii hiyo? Katika utafiti huu wahojiwa waliweza kueleza umuhimu ambao huambatana na maana ya jina linalotewa kwa mtu kulingana na maana na kigezo kilichotumika. Kwa ujumla data za utafiti huu zimedhihirisha kuwa majina ya Kimatengo yana maana za kiishara zinazoambatana na umuhimu katika jamii hiyo kulingana na utamaduni, historia na mazingira ya jamii hiyo. Sehemu

ifuatayo inawasilisha data zilizopatikana katika utafiti huu kuhusu umuhimu wa maana za majina katika jamii ya Wamatengo:

### 4.5.1 Kutambulisha Utamaduni wa Jamii

Moja, maana hizo zimedhihirisha kuwa majina ya watu yana mchango mkubwa sana katika kuutambulisha na kuuhifadhi na kuuendeleza utamaduni wa jamii ya Wamatengo. Majina ya watu katika jamii ya Wamatengo ambayo mtafiti ameyaorodhesha katika utafiti huu yana umuhimu mkubwa kuhifadhi, kutambulisha na kuendeleza utamaduni wa jamii ya Wamatengo mfano majina ya ukoo kama vile Komba, Mapunda, Nyoka na Nguruwe.Vilevile majina kama Malelu, Kalyoba na Kahweba huendeleza kuhifadhi matukio mbalimbali katika utamaduni wa Kimatengo.

### 4.5.2 Kuhifadhi Historia ya Jamii

Pili, maana za majina ya watu zimedhihirisha kuhifadhi historia na matukio mbalimbali yaliyotokea kwa mtu mmoja mmoja au jamii.Kwa mfano jina Kangondu lenye maana ya aliyezaliwa kipindi cha vita au Malelu lenye maana kuwa amezaliwa wakati wazazi wake wakiwa na majo cha ndugu yao. .Aidha, jina Kanzala lenye maana ya aliyezaliwa kipindi cha njaa katika jamii yao, limehifadhi historia kuwa jamii hiyo ilikumbwa na tatizo la njaa.

### 4.5.3 Kuadibu

Tatu, maana za majina ya watu zinapofahamika husaidia kutahadharisha juu ya tabia mbaya walizonazo baadhi ya watu ili jamii ichukue tahadhari dhidi yao.Kwa mfano, jina la Sindukumoso linamaana ya mwanaume mwenye tabia ya kupenda kufanya

mapenzi na wanawake wengi (umalaya) au mpyoli mtu mwenye tabia ya kuchonganisha (kugombanisha) watu mbeya au mwongo, hivyo tabia hii huidharisha jamii na hivyo jamii inatahadharisha tabia hii haifai kwa kuwapa wanajamii ya Wamatengo majina yanayowakilisha tabia mbaya.

### 4.5.4 Kuendeleza Utamaduni wa Utani

Nne, maana za majina ya watu zimedhihirisha kuendeleza utani baina ya wanajamii. Mulokozi (1996:49) anaeleza yafuatayo kuhusu utani:

> "Mila ya utani imeenea sana katika makabila mengi ya Afrika Mashariki. Aghalabu watani wanapokutana hutaniana kwa maneno (na hata vitendo), huku wakizingatia masharti yanayotawala uhusiano wao wa kiutani''.

Watu hupewa majina ya utani kwa sababu mbalimbali kama vile kazi anayoifanya mtu, kwa mfano jina la Kahomba kumtania mtu anayefanya kazi ya kuvua samaki lenye maana kasamaki kadogo. au Kahosu ni jina la utani pia ambalo hutumia jamii ya Wamatengo kumtania mtu katika jamii kuonesha kuwa hanakitu au ameishiwa kwa kipindi ambacho alikuwa hanafedha wenzao wanafedha za kufanyia matumizi.

### 4.5.5 Kuonesha Hisia

Tano, maana za majina ya watu katika jamii ya Wamatengo husaidia kutunza hisia wanazokuwa nazo Wazazi au wanajamii pamoja na mafumbo. Hisia hizi huweza kudhihirishwa kwa njia ya mafumbo. Hivyo, majina ya namna hii huweza kuitwa fumbo-jina.

Mulokozi (1996:41) anaeleza kuwa majina mengi ya watu, mifugo, vijiji, vitu, n.k. katika makabila yetu huwa ni aina ya mafumbo ambayo hudokeza hali, tukio au funzo fulani. Kwa mfano, mtoto aliyezaliwa na dosari za maumbile huitwa 'njiti'. Majina katika jamii ya Wamatengo kama vile Kasiki lenye maana ya mtu aliye zaliwa njiti yaani kabla ya muda wake au Libambo lenyevmaana ya mtu ambaye mwanaume mwenye umbile kubwa au mnene kulinganisha na wengine.

### 4.5.6 Kutofautisha Mtu na Mtu

Sita, maana za majina ya watu zimedhihirisha tofauti baina ya mtu mmoja na mwingine, yaani majina ya watu humtofautisha mtu mmoja na mwingine, kwa mfano si wanaume wote waliopewa jina la Kagunila. Aidha, si wasichana wote waliopewa jina la Kasiki au Rujendu au Kapusanga. Hivyo, jina husaidia katika utambulisho wa mtu binafsi. Majina ambayo watu wamepewa kwa sababu ya tabia walizonazo kama vile Rujendu au Kapenuka kuwa na tabia ya mtembezi. Huonesha hali ya maumbile waliyonayo kama vile Kapehi yaani mtu mwembamba au Kajipi au Kasiki yaani mtu mfupi, au kazi wanazozifanya kama vile Ponda yaani mtu anayefanya kazi ya uhunzi, husaidia kutambulisha tabia au maumbile au kazi anayefanya.

### 4.5.7 Kuelimisha

Saba, maana za majina ya watu huiadibu jamii, yaani huifundisha jamii mwenendo mwema au tabia njema, kama vile majina wanayopewa watu ili kuwasifia au kuwakosoa. Kwa mfano jina Kapenga lenye maana ya mtu mwenye kupokeapokea wageni na kuwaandalia chakula, linahimiza ukarimu kwa wageni. Jina Kalema lenye maana ya mtu anayependa kulima, Jina Rujendu na Sindukumoso linakosoa na

kuionya jamii kuhusiana na tabia hiyo mbaya jamii iepukane na tabia mbaya kwa kuepuka kupewa majina kama haya katika jamii ya Wamatengo.

### 4.5.8 Kukuza Lugha

Nane, maana za majina ya watu zimedhihirisha namna majina yanavyokuza lugha. Majina ni sehemu ya maneno ya lugha husika. Kwa kuwa majina mengi huwa na maana hivyo basi kadiri yanavyoundwa ndivyo yanavyokuza lugha hiyo. Mfano wa majina hayo jina Kahosu lenye maana ya mtu mwenye kipato cha chini na Kanzika lenye maana ya mtu aliyezaliwa peke yake. Kasiki linamaana mtu mfupi hivyo majina haya hukuza lugha ya Kimatengo na lugha ya Kiswahili pia ambayo ina Ubantu ndani yake. Kwa hakika, maana za majina ya watu katika jamii ya Wamatengo zimedhihirisha kuwa na umuhimu mkubwa sana kwa jamii hiyo.

## 4.6 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amefanya uwasilishaji na uchambuzi wa data ili kukamilisha malengo ya utafiti huu. Uchambuzi huu umedhihirisha kwamba majina mengi wanayopewa watu katika jamii ya Wamatengo huwa na maana, ama fiche au iliyo bayana. Aidha yapo mambo mbalimbali yanayosababisha mtu kupewa jina fulani, na maana ya jina hilo huwa na umuhimu katika jamii hiyo kwa kuzingatia sababu husika mfano sababu ya maumbile au rangi, sababu ya tabia walionao wanajamii katika jamii ya Wamatengo au matukio mbali mbali yaliyotokea katika jamii mfano njaa au vita vya wenyewe kwa wenyewe katika koo.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inahusu muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo. Kipengele cha muhtasari kinabainisha kwa ufupi mambo yaliyojadiliwa katika utafiti huu. Kipengele cha hitimisho kinafunga mjadala wa matokeo ya utafiti na kipengele cha mapendekezo kinatoa ushauri wa mambo yanayoweza kuchunguzwa zaidi katika tafiti zijazo.

## 5.2. Muhtasari wa Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza vigezo vya utoaji wa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo. Katika kufanya utafiti huu, mtafiti aliongozwa na malengo mahususi matatu ambapo lengo la kwanza lilikuwa ni kubainisha vigezo vinavyotumika kutoa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo. Lengo la pili ni kufafanua maana za kiishara zinazofumbatwa na majina ya watu katika jamii ya Wamatengo. Lengo la tatu ni kujadili umuhimu wa maana za majina ya watu katika jamii ya Wamatengo.

Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data za utafiti ni usomaji makini, usaili na mahojiano ya vikundi. Pia, utafiti huu ulitumia mkabala wa maelezo katika uwasilishaji wa data. Uwasilishaji na uchanganuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Semiotiki ambayo huzingatia mifumo ya ishara mbalimbali kulingana na uhusiano uliopo baina ya kiwakilishi na kitajwa. Kupitia nadharia hiyo, mtafiti ameweza kubainisha vigezo vinavyotumika kutoa majina ya watu, kufafanua maana za kiishara zinazofumbatwa katika majina na kujadili umuhimu wa maana za majina ya watu

katika jamii ya Wamatengo. Matokeo ya utafiti kwa mujibu wa malengo mahususi ya utafiti huu yamebainishwa na kujadiliwa katika sura ya nne ambapo kwa muhtasari yanaonesha kama ifuatavyo:

### 5.2.1Vigezo Vinavyotumika Kutoa Majina

Utafiti huu umebaini kuwa kuna vigezo mbalimbali ambavyo hutumika kutoa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo. Vigezo hivyo ni pamoja na tabia au sifa aliyo nayo mtu, hisia au imani za wazazi, mazingira yaliyowazunguka na matukio yaliyojiri wakati mtoto anazaliwa. Vigezo vingine ni kazi aliyonayo mtu, maumbile au rangi ya mwili, kipindi mtoto alichozaliwa na mahali alipozaliwa mtoto huyo. Hata hivyo, utafiti umebaini kuwa mtoto anaweza kupewa jina la kuzaliwa na baadaye anapokuwa mkubwa hupewa jina linalofungamana na imani ya dini yake au wazazi wake.

### 5.2.2 Maana za Kiishara Zinazofumbatwa katika Majina

Utafiti huu umebaini kuwa kuna maana za kiishara zilizofumbatwa na majina ya watu katika jamii ya Wamatengo.Maana hizo zinaashiria tabia au sifa aliyo waliyo nayo wazazi wa mtoto wakati alipozaliwa. Pia, maana za majina huashiria hisia au imani za wazazi wa mtoto kama vile dini au imani za jadi. Aidha, huashiria mazingira yaliyowazunguka wazazi wa mtoto na matukio yaliyojiri wakati mtoto anazaliwa. Ishara nyingine zinaashiria kazi za watu katika jamii mtoto alipozaliwa, maumbile na rangi ya mwili. Vilevile, maana nyingine zinaashiria kipindi fulani cha historia ambacho mtoto amezaliwa na pia mahali alipozaliwa mtoto huyo.

### 5.2.3 Umuhimu wa Maana za Majina

Utafiti huu umebaini kuwa kuna majina ya watu yana umuhimu mkubwa katika jamii ya Wamatengo. Miongoni mwa umuhimu wa maana za majina ya watu ni kuhifadhi utamaduni wa jamii, kuutambulisha na kuulinda utamaduni wa jamii. Umuhimu mwingine ni kuadibu wanajamii, kuonesha hisia alizonazo mwanajamii, kutofautisha baina ya mtu mmoja na mwingine, kuelimisha jamii na kukuza lugha inayohusika. Pamoja na umuhimu huo, utafiti umebaini kuwa umuhimu mkubwa wa majina ya watu ni kumtofautisha mtu na mtu katika jamii.

## 5.3 Hitimisho

Utafiti huu ulichunguza vigezo vya utoaji wa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo. Matokeo ya utafiti yamedhihirisha kuwa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo hayatolewi kiholela bali hutolewa kwa kuzingatia vigezo maalumu. Pamoja na vigezo hivyo, imani za dini za wazazi na maendeleo ya sayansi na teknolojia kwa kiasi fulani yameanza kuviathiri vigezo hivyo. Aidha, katika majina ya watumna maana za kiishara zinazofumbatwa ndani ya majina hayo ambapo ishara hizo huakisi historia na maisha ya kila siku katika jamii ya Wamatengo. Pia, maana za majina ya watu zina umuhimu mkubwa katika jamii ya Wamatengo kwa sababu maana hizo hutambulisha na kuhifadhi utamaduni wa jamii ya Wamatengo. Katika muktadha huo, ni dhahiri kuwa utafiti huu unatoa mchango mkubwa katika taaluma ya isimu hususani katika tawi la semantiki. Hivyo basi, utachangia katika tafiti za lugha za Kibantu na kuwa kichocheo cha kufanyika tafiti nyingizaidi zinazohusiana na mada hii.

## 5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu kama tafiti nyingine za sayansi jamii hatuwezi kusema kuwa umekamilika. Kwa hiyo, utafiti huu unaweza kuchukuliwa kama juhudi mojawapo ya kutafiti vigezo vya utoaji wa majina ya watu katika jamii mbalimbali za Afrika. Kwa hiyo, mtafiti anatoa mapendekezo yafuatayo:

Mosi, kwa kuwa utafiti huu ulijikita katika vigezo vya utoaji wa majina ya watu katika jamii ya Wamatengo. Kwa hiyo utafiti kama huu unaweza kufanywa katika jamii nyingine, hasa ikizingatiwa kwamba jamii hutofautiana na kuhusiana kiutamaduni, shughuli zao za kiuchumi na makazi yao kijografia. Pia, kwa kuwa utafiti huu ulijihusisha na majina ya watu, utafiti mwingine unaweza kufanywa kuhusiana na majina ya miji, wilaya, mabango, wanyama, miti, ndege na kadhalika.

Pili, wazazi katika jamii waendelee kuwapa watoto wao majina yenye asili ya jamii zao ili kuendeleza na kuhifadhi mila, desturi na utamaduni wa jamii hiyo. Kwani mtafiti alibaini kuwa watoto wengi wanaozaliwa hivi sasa hawapewi majina yanayohusiana na jamii yao. Hivyo, inawawia vigumu watoto hao kufahamu maana za majina hayo na pia baada ya muda majina hayo yatapotea kabisa katika jamii ya Wamatengo. Hali hii inatokana na mwingiliano wa watu wenye tamaduni nyingine hususani kama kabila la Wangoni na Wanyasa ambayo ni makabila ya jirani. Vile vile hamahama za watu wa jamii kutoka vijijini kwenda mijini na utumizi wa Kiswahili katika shughuli mbalimbali kielimu, kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa ndani ya nchi imepelekea watoto wanaozaliwa katika jamiiya Wamatengo kupewa majini ambayo sio ya asili wakidai wanaenda na wakati. Pia shughuli za dini, kama

vile Ukristo na Uislamu zimechangia katika imani hizi kubatiza watoto majina ya kidini zaidi na kuachana naya majina ya utamaduni wa jamii ya Wamatengo.

**MAREJEO**


Ali, H. H. (2014). Kuchunguza Dhima ya Fasihi ya Majina ya Mtaa Mjini Unguja. Tasnifu ya Uzamili ya Kiswahili Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania

BAKIZA, (2010). *Kamusi ya Kiswahili Fasaha*. Nairobi Oxford University Press.

Beidelman, T. O. (1974) ‘’*Kaguru Names and Naming*’’ katikaJournal of Anthropological Research, 30:281-93. The University of Chicago Press.

Best, J. W. (1981) *Research in Education,* fourth edition, New Jersey: Prentice-Hall, Inc.

Beattie, J. (1957). *Nyoro Personal Names*” katika Uganda Journal, 21:99-106.

Buberwa, A. (2010). *Investigating Socialinguistic Aspects of Place Names. The case of Ruhaya in North-western Tanzania*. Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Chiumbo.A (2016) *Maana za majina ya watu katika jamii ya Wayao*. Tasinifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Chulk, O. (1992). *Names from African: Their Origin, Meaning and Pronounciation*. Chicaco: John Benjamin Publishing.

Chandler, D. (2002) *Semiotics for Beginners.* Aberystwyth: Aberystwyth University.

Denice, S. (2011) *Haja ya Kuundwa Kamusi ya Majina ya Watu ya Asili katika Jamii ya Wahaya*. Tasnifu ya shahada ya uzamili (haijachapishwa). Chuo kikuu cha Dar-es-Salaam.

Enon, J. C. (1998), *Educational Research, Statistics and Measurement*, second edition, Kampala: Makerere University.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004), *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*, Nairobi: Phoenix Publishers.

Hornby, A. S. (2006), *Oxford Advanced Learner's Dictionary of Current English*, Seventh edition. Oxford: Oxford University Press .

*hltps://www.tra.go.tz/images/documents/postcode/ruvuma.pdf au Sensa ya 2012, Ruvuma-Mbinga District council.*

Kapinga, M.C (1983). Taasisi ya Uchunguzi wa

Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Katakami, H. (1997)'' *Personal Names and Modesof* A*ddress Among the Mbeere''* katikaAfrican Study Monographs,18(3,4):203-212.

Kihore, Y. M., na Chuwa, A. R. (2009). Kiswahili Katika Karne ya Ishirini na Moja. Chuo Kikuu Dar es Salaam.Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B. na Msanjila, Y.P. (2009). Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Kombo, D. na Tromp, D. L. A. (2006), *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications.

Kothari, C. R. (2004), *Research Methodology: Methods and Techniques*, Second revised edition, New Delhi : New Age International (P) Ltd, Publishers.

Kumar .R. (2005), *Research Methodology : A Step-by Step Guide for Beginners*, Second edition, London: Sage Publications.

Kress, G. (1985). Linguistic Process in Socio-culture Practice: Victoria Deakin University Press.

Kuranchie, A. (2012). Student"s Nick Names: Their Source and Effects on Learning. Faculty of Education, Catholic University College of Ghana. Journal of Education and Practice. 3(14). 23- 41.

LoBiondo-Wood,G.& Haber, J. (1998), *Nursing Research: Methods, Critical Appraisal and Utilization* (4th ed.) St.Louis , Mo: Mosby.

Lyons, J. (*1995)*. Linguistic semantics: An introduction.

Cambridge, England: Cambridge University Press.

Manyasa, J. (2009), *Investigating the Basis of Naming People in Kisukuma*, M.A. (Linguistics) Dissertation, University of Dares-salaam.

Massamba, D. P. B. (2009), *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*, chapa ya pili, Dar-es-Salaam: TUKI.

Matinde, R. S. (2012), *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia*, Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Mbiti, J. S. (1991) *Introduction to African Religion*, second edition, Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mdee, J. S. (2010) *Nadharia na Historia ya Leksikografia,* chapa ya tatu, Dar-es-salaam : TUKI

Mdee, J. S., Njogu, K. na Shafi, A (2013) *Kamusi ya Karne ya 21,* toleo la pili, Nairobi: Longhorn.

Mgullu, R. S. (1999) *Mtala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia yaKiswahili*. Nairobi: Longhorn.

Mligo, E. S. (2012) *Jifunze Utafiti,* Dar-es-salaam: Ecumenical Gathering (EGYS).

Msanjila, Y. P, Kihore, Y. M na Massamba, D. P. B. (2009) *Isimu Jamii Sekondari na Vyuo* , Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. (1996) *Fasihi ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Munyao, K.M. (2006) The Morph Syntax of Kikamba Verb Derivations: A Minimalist

Approach. The University of Nairobi, Nairobi, Kenya.

Musso, M. (1968), *MUKWAVA na Kabila Lake*. Arusha: Eastern Africa Publications Ltd.

Musyimi, D. M. (2011), *Maana za Majina ya Watu katika Jamii ya Wakamba*, Tasnifu ya shahada ya uzamili, Kenyatta University.

Mutembei, A.K (2009) *UKIMWI katika fasihi ya Kiswahili*, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili chuo kikuu Dar Es Salaam.

Ngunga, A. S. A. (1995), *Phonetics and Phonology of Vowel Length in Ciyao*, M.S. Berkeley: University of Califonia.

Ngunga, A. S. A. (1997), *Class 5 Allomorphy in Ciyao*, University of Califonia.

Olenyo, M. M. J. (2011) ''*What is in a Name? An Analysis of the Semantics of Lulogooli Personal Names''* katikaInternational Journal of Humanities and Social science, Vol. I, no.20.

Polit, D. F. na Hughler, B.P. (1998) *Nursing Research: Principles and Methods*, 6th edition. Philadelphia: Lippincott.

Pons, V. ed (1992) *Introduction to Social Research.* Dar-es-salaam : Dar-es-salaam University Press.

Resani, M. (2014) *Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili*, Dar: Karljamer Print Technology.

Saussure, F. (1966) *Course in General Linguistics* (translated by Wade Baskin). New York: Mc Graw-Hill Book Company.

Scholes, R. (1982) *Semiotics and Interpretation*, New Haven: Yale University Press.

Sitati, V. W. (2007) *Comprehensive Names Dictionary*. Nairobi: Sas Enterprise.

Starks, D.,na Taylor-Leech, K. (2011).Research Project on Nicknames and

Adolescent Identities.New Zeland Studies in Applied Linguistics.

TATAKI (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Toleo la tatu, Dar: Oxford University Press.

TUKI (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*, Dar-es-Salaam: TUKI.

Williman, N. (2011). *Research Methods*; The Ba London and New York, Routledge

Taylor and Francis Group.

Whiteley, W. H. (1966), *A Study of Yao Sentences*, Oxford : Oxford University.

World Book Encyclopedia (1987), *N-O,''Name''*, Volume 14, Chicago:World Book,Inc.

Whiteley, W. H. (1966). A Study of Yao Sentences. London: Oxford University

# VIAMBATANISHO

## KIAMBATANISHO1 :  HOJAJI

A.TAARIFA ZA MHOJIWA

(I).Jina…………………………………………………..

(II). Jinsia: mwanamume/mwanamke (kata isiyostahiki)

(III).Mahali unapoishi……………….. (andika jina la kijiji)

(IV).Kazi…………………………………………………

B.MASWALI KUHUSU UTAFITI

1. Orodhesha majina kumi (12) ya asili ya watu katika jamii ya Wamatengo na maana zake:

| NA. | JINA | MAANA |
|---|---|---|
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| 11 | | |
| 12 | | |

2. Orodhesha majina ishirini (20) ya asili ya watu katika jamii ya Wamatengo yanayo onesha sifa au tabia na maana zake:

| NA. | JINA | JINSIA | MAANA |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |
| 7 | | | |
| 8 | | | |
| 9 | | | |
| 10 | | | |
| 11 | | | |
| 12 | | | |
| 13 | | | |
| 14 | | | |
| 15 | | | |
| 16 | | | |
| 17 | | | |
| 18 | | | |
| 19 | | | |
| 20 | | | |

3.Orodhesha majinaishirini (20) ya asili ya watu katika jamii ya Wamatengo yanayo onesha rangi au maumbile na maana zake:

| NA. | JINA | JINSIA | MAANA |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |
| 7 | | | |
| 8 | | | |
| 9 | | | |
| 10 | | | |
| 11 | | | |
| 12 | | | |
| 13 | | | |
| 14 | | | |
| 15 | | | |
| 16 | | | |
| 17 | | | |
| 18 | | | |
| 19 | | | |
| 20 | | | |

4. Orodhesha majina ishirini (20) ya asili ya watu katika jamii ya Wamatengo yanayo onesha matukio na maana zake:

| NA. | JINA | JINSIA | MAANA |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |
| 7 | | | |
| 8 | | | |
| 9 | | | |
| 10 | | | |
| 11 | | | |
| 12 | | | |
| 13 | | | |
| 14 | | | |
| 15 | | | |
| 16 | | | |
| 17 | | | |
| 18 | | | |
| 19 | | | |
| 20 | | | |

5. Orodhesha majinaishirini (20) ya asili ya watu katika jamii ya Wamatengo yanayoonesha misimu na maana zake:

| **NA.** | **JINA** | **MAANA** |
|---|---|---|
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| 11 | | |
| 12 | | |
| 13 | | |
| 14 | | |
| 15 | | |
| 16 | | |
| 17 | | |
| 18 | | |
| 19 | | |
| 20 | | |

6. Orodhesha majina ishirini (20) ya asili ya watu katika jamii ya Wamatengo yanayoonesha mahali na maana zake:

| **NA.** | **JINA** | **MAANA** |
|---|---|---|
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| 11 | | |
| 12 | | |
| 13 | | |
| 14 | | |
| 15 | | |
| 16 | | |
| 17 | | |
| 18 | | |
| 19 | | |
| 20 | | |

5.Orodhesha majina ishirini (20) ya asili ya watu katika jamii ya Wamatengo yanayoonesha hisia na imani ya jamii na maana zake:

| **NA.** | **JINA** | **MAANA** |
|---|---|---|
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| 11 | | |
| 12 | | |
| 13 | | |
| 14 | | |
| 15 | | |
| 16 | | |
| 17 | | |
| 18 | | |
| 19 | | |
| 20 | | |

2. Nini sababu ya watu kupewa majina hayo?

3. Majina hayo yana umuhimu gani katika jamii yako?

## KIAMBATISHO 2: MASWALI YA USAILI (MAHOJIANO)

1.Mahojiano hayo kwa ajili ya kupata maana ya majina ya Wamatengo

2.Unatakiwa kujibu maswali yafuatayo kwa uelewa wako

(i) Unaitwa nani…………………………………………………

(ii)Umri wako…………………………………………………

(iii)Jinsia yako………………………………………………

(iv) kata unayoishi inaitwa……………………………………

(v)Kijiji unachoishi kinaitwaje…………………………………..

3.Taja majina ishirini (20) asili ya watu jamii ya Wamatengo yenye maana wanayo wapatia watoto wao au watu katika jamii yao yanayo onesha tabia au sifa

| NA. | JINA | JINSIA | MAANA |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |
| 7 | | | |
| 8 | | | |
| 9 | | | |
| 10 | | | |
| 11 | | | |
| 12 | | | |
| 13 | | | |
| 14 | | | |
| 15 | | | |
| 16 | | | |
| 17 | | | |
| 18 | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 19 | | | |
| 20 | | | |

4.Taja majina kumi (10) ya asili ya Wamatengo wanayowapatia watoto wao ambayo yanaonesha matukio mbalimbali katika jamii na maana yake.

| NA. | JINA | JINSIA | MAANA |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |
| 7 | | | |
| 8 | | | |
| 9 | | | |
| 10 | | | |

5.Taja majina kumi (10) asili ya Wamatengo wanayowapatia watoto au watu katika jamii yanayoonesha mahali na maana ya majina hayo

| NA. | JINA | JINSIA | MAANA |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |
| 7 | | | |
| 8 | | | |
| 9 | | | |
| 10 | | | |

6.Taja sababu tano (5) ambazozimepelekea jamii ya Wamatengo za kuwapatia watoto wao majina majina asilia .

7.Taja umuhimu wa kuwapatia au kuwapa watoto majina asili katika jamii ya Wamatengo na yenye maana.

Asante kwa ushirikiano

**KIAMBATANISHO 3: RAMANI YA MKOA WA RUVUMA WILAYA YA MBINGA ENEO AMBALO JAMII YA WAMATENGO WANAPATIKANA**




Rejea chanzo cha taarifa:*hltps://www.tra.go.tz/images/documents/postcode/ruvuma.pdf au Sensa ya 2012, Ruvuma-Mbinga District council.*